**LUGHA** yasababisha mahakama kuamuru kesi aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa kusikilizwa upya



UKURASA 5

**WAAJIRI** sekta binafsi watiwa kibano kima cha chini mshahara

UKURASA 3



ama
AFYA NA MAZINGIRA

Kitisho cha joto kali kinapolipuka tena Ulaya na Asia sasa ni nyuzi 50

Mchawi kudorora huduma za afya vituoni, zahanati hospitalini huyu hapa

Rukwa sasa yaelekea kuandika historia kutokomeza mimba na ndoa za utotoni

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Julai 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581377

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Paroko auawa kikatili kanisani



**MUUAJI** naye auawa na wananchi... *Endelea ukurasa wa 2*

## Nape amvaa Lissu kisa lugha dhidi Samia

UKURASA 2



Tundu Lissu

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye

UKURASA WA 5

### USHIRIKIANO TANZANIA NA UFARANSA WAONGEZA WATALII

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Damas Ndumbaro, amesema ushirikiano wa Tanzania na Ufaransa umesaidia kuleta maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwamo kuongeza watalii kila mwaka nchini...

UKURASA WA 8

### MKENDA AMULIKA UBORA WA VYUO VIKUU

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameitaka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kuongeza jitihada katika udhibiti wa ubora wa vyuo vikuu ili kuhakikisha azma ya kuwa na mitaala inayojibu mahitaji...

### TMA yahadharisha El-Nino, mikoa tisa yatajwa kuathirika

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAFUNGUKA UJIO MAKUDUBELA 'SKUDU' UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Paroko auawa kikatili kanisani

**Na Allan Isack,** KARATU

PAROKO ameuawa. Wananchi walioshindwa kudhibiti hasira zao, wamemuua muuaji wa kiongozi huyo wa kiroho.

Ni tukio lililotokea jana alfajiri Paroko wa Parokia ya Karatu, Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, mkoani Arusha, Padri Pamphili Nada, alipouawa na kijana wa kiume anayedaiwa kuwa na matatizo ya akili.

Inadaiwa kuwa paroko huyo aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito na kijana ambaye anadaiwa alilazimisha kuingia kanisani ili kusali.

Kijana huyo aliyetajwa kwa jina ya Romani Leonard (30), anadaiwa kuwa baada ya kufanya mauaji hayo, naye aliuawa na wananchi wenye hasira waliofika kanisani hapo baada ya paroko kuawa.

Kamanda wa Polisi Mkoa Arusha, Justine Masejo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, akiwa na ufafanuzi ufuatao:

"Padri alifariki wakati anapelekwa hospitalini na mtuhumiwa aliuawa na wananchi wenye hasira baada ya kupata taarifa za tukio hilo," alisema.

Wakazi wa eneo kulikofanyika mauaji hayo, akiwamo Rehema Baha, walisema kuwa jana alfajiri, walisikia mtu akipiga kelele kutaka kuingia kusali, ndipo Padri Nada alipotoka na kumwambia mlinzi amfungulie mlango.

"Baada ya kuingia ndani (kanisani) na akiwa na padri tu, ndipo alichukua chuma cha mlango na kumpiga padri, alifariki dunia wakati anakimbizwa hospitalini," alidai.

Naye Peter Yohana, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema kutokana na tukio hilo, kengele ya kanisa ilipigwa na wananchi kukusanyika na baada ya kupata taarifa hizo walianza kumpiga kijana huyo na kusababisha kifo chake.

"Tunamfahamu huyu mtu, anatoka Kijiji cha Gekum Rambo na amekuwa Karatu kwa muda sasa," alidai Yohana.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kushoto), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wakala wa Vyuo Vikuu Nje ya nchi ya Global Education, Abdulmalimak Mollel (kulia), baada ya kutembelea banda la taasisi hiyo katika maonyesho ya 18 ya Vyuo Vikuu, Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia yanayosimamiwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nape amvaa Lissu kisa lugha dhidi ya Samia

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Nape Nnauye, amemkosoa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kwa madai ya kutumia lugha aliyoiita chafu kumkosoa Rais Samia Suluhu Hassan.

Juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kongamano la majadiliano ya Ripoti ya Tume ya Haki Jinai, Nape alieleza kukerwa na kile alichodai namna Lissu alivyopinga mawazo ya Rais Samia kwa kutumia lugha isiyo na staha.

"Leo (juzi), nilikuwa ninasikiliza mjadala mmoja, nikawa ninasikiliza clip (kipande cha sauti au video iliyorekodiwa) moja ya mjomba wangu.

"Kuna mjomba wangu mmoja anatoka Singida, akawa anakosoa mawazo ya Rais, ya kuwajumlisha watu wanaokosoa kwenye mchakato wa kuboresha mambo.

"Kukosoa sio kubaya, lakini alikuwa anatumia maneno ya ovyo sana, anasema hivi 'haya mawazo ya Rais ni matope, tena akatumia lugha chafu ya Kiingereza - presidential rubbish'.

"Sasa ndugu zangu Watanzania, huyu Rais wetu ni mstaarabu. Ametupa fursa ya kuongea, miaka miwili mitatu nyuma ninyi wenyewe ni mashahidi tusingefika hapa," Nape alisema.

Waziri huyo ambaye hadi hatua hiyo alikuwa hajaweka bayana jina la kiongozi aliyemlenga, aliendelea:

"Na mjomba wangu, kaenda kuchanganya mambo, anasema Rais anataka watu waende kutoa mawazo kwenye bandari, wakati siyo kweli, ni kwenye Tume ya Mipango. Lakini ukiacha yeye (Rais Samia) kuwa kiongozi mkubwa, pia ni mama wa kitanzania."

Waziri huyo alisema kitendo cha 'mtu mzima' kutoa maneno makali dhidi ya Rais hadharani, kinajenga watoto wasio na heshima kwa viongozi.

"...kesho atatukanwa mama yako. Tunataka hawa watoto waamini ukipishana na mzazi wako utamwambia hiyo ni akili ya matope? Ndiko tunakotaka kuipeleka Tanzania?" Nape alihoji.

Licha ya kutomtaja aliyemlenga, Nape alisema kuwa alipopigwa risasi na kwenda kutibiwa Kenya, Rais Samia ndiye alikuwa kiongozi pekee kutoka mamlaka ya juu ya serikali aliyekwenda kumwona hospitalini.

Ni kauli iliyothibitisha kwamba malalamiko hayo ya Nape yalimlenga Lissu ambaye miaka sita iliyopita, alishambuliwa kwa kupigwa risasi 38 nyumbani kwake jijini Dodoma.

"Akiwa Rais, (Samia) akafunga tena safari kwenda Ubelgiji alikokuwa amekimbilia akamwita, akampa pole hadharani, akamwambia 'mdogo wangu pole, sasa rudi nyumbani' kwa akili hiyohiyo anayoiita ya matope?

"Lakini ni Rais huyu ndiye akasema 'mlifungiwa kufanya mikutano yenu, nendeni mkafanye'. Ile rukhsa ni kwa hii akili ya matope? Ni kweli kwamba tunataka watoto wetu waanze kuwatukana wazazi wao?" Nape alihoji.

Alisema kutukanwa kwa mwanamke mmoja wa nchi ni sawa na kutukanwa kwa wazazi wote.

"Tukusoane, turekebishane, tutoe maoni wala tusitukanane. Mwalimu alitufundisha tushindane kwa hoja, hasa inapokuwa ni Rais wa nchi yetu maana yeye ni sura yetu sote," alishauri.

# Shirika la Marekani lasaidia kituo vifaa kinga vya mil. 50/-

**Na Halfani Chusi**

SHIRIKA lisilo la kiserikali kutoka nchini Marekani, linaloshughulikia afya, elimu na maendeleo ya kilimo (AHEAD Inc), limetoa msaada wa vifaa kinga vyenye thamani ya Sh. milioni 50 katika Kituo cha Afya Maruku, Wilaya ya Bukoba Vijijini mkoani Kagera.

Shirika hilo, limetoa msaada huo baada ya kupata habari kuwa baadhi ya wafanyakazi wa afya katika kituo hicho, waliambukizwa ugonjwa wa virusi vya Marburg na mmoja wao kupoteza maisha.

Mjumbe wa Bodi ya Shirika hilo, Dk. Bryon Burks, alisema wanajihusisha katika shughuli za ujenzi wa miundombinu, kusaidia kuchangia fedha kwa ajili ya vifaa tiba na dawa katika kituo hicho.

Alisema kwa muda huo, walifanikiwa kuwatambua na kuwatenga waliopata maambukizi ya ugonjwa wa Marburg, ili kudhibiti kuenea maeneo mengine akisisitiza kuwa bila kuwa na hospitali mgonjwa angeweza kufia nyumbani na kuwaambukiza wanaomhudumia.

Mjumbe huyo alisema, vifaa walivyosaidia ni pamoja na barakoa 2,000, maboksi 31,200 ya glovu za mkononi na mavazi rasmi yatakayovaliwa katika chumba cha upasuaji.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Dk. Bandioti Gavyole, alisema vifaa hivyo vitasaidia kuwakinga wafanyakazi wa afya na kuwaongeza moyo wa kujiamini wanapotoa huduma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Dk. Donna Williams, alisema shirika lao, litaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na kituo hicho kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa zaidi katika maeneo ya vijijini na Tanzania kwa ujumla.

Alisema, pia wametoa msaada wa kompyuta 10 na kugharamia mfumo wa intaneti katika Shule ya Sekondari Maruku ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa njia ya mtandao jambo lililoungwa mkono na Mkuu wa shule hiyo, Farida Kamanyile, ambaye alisema uelewa wa wanafunzi kutumia kompyuta kwa sasa umeongezeka.

Wiki iliyopita, Shirika hilo liliwaleta wafanyakazi 27 wa kujitolea kutoka nchini Marekani, wakiwamo wauguzi kutoka Shirika la Wauguzi la New York (NYSNA), watabibu na madaktari wa meno ambao waliwahudumia wagonjwa zaidi ya 700 kwa siku mbili mfululizo bure.

Shirika hilo, lilianzishwa na Dk. Irving Williams na mke wake mwaka 1985 pamoja na watoto wao wanne waliishi na kufanya kazi Mwanza kati ya mwaka 1970, katika Hospitali ya Bugando na Shule ya Msingi Nyakahoja.

HABARI KITAIFA

# Biteko ataja mikakati 3 madini kuchangia pato la taifa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ametaja mikakati mitatu iliyowekwa na serikali ili kuhakikisha sekta ya madini inakuwa na mchango mkubwa katika pato la taifa, pamoja na kuvutia wawekezaji zaidi ifikapo mwaka 2025.

Mikakati hiyo kwanza ni serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kujielekeza kwenye utafiti kwa kushirikiana na sekta binafsi, pili ni utoaji wa leseni za uchimbaji madini kwa watu wote bila ubaguzi, tatu ni kupeleka miundombinu ya kurahisisha biashara maeneo ya migodini.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa wadau wa madini uliolenga kupata ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili sekta ya madini, nini kifanyike ili iwe na mchango mkubwa katika pato la taifa.

Alisema, malengo ya serikali ni kuhakikisha sekta ya madini inachangia zaidi ya asilimia 10 katika pato la taifa ifikapo mwaka 2025, pamoja na kuvutia wawekezaji zaidi.

"Wadau wa madini wamekuwa wakikumbwa na changamoto mbalimbali ikiwamo za kikodi, kiusimamizi, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kodi ya ubia pamoja na baadhi ya sheria zinazoingiliana na sekta ya madini," alisema Biteko.

Alisema serikali imesikia kilio cha wadau hao, changamoto nyingi zimeanza kupatiwa ufumbuzi na hivi sasa wawekezaji katika sekta ya madini wametengenezewa mazingira mazuri.

Kuhusu usalama katika migodi, Biteko alisema miaka ya nyuma kulikuwa kunatokea ajali nyingi katika migodi, lakini kwa miaka ya sasa imepungua.

Alisema hatua hiyo imechagizwa na hatua ya serikali kuweka utaratibu wa kusimamia sheria ya usalama mahali pa kazi katika migodi, pamoja na kutoa elimu ya usalama kwa wachimbaji.

Kadhalika, hivi sasa kampuni nyingi za uchimbaji madini zinatumia vifaa vya kisasa katika uchimbaji kutofautisha na miaka ya nyuma waliyokuwa wanatumia vifaa duni.

Mwenyekiti wa Chemba ya Madini Tanzania (TCM), Mhandisi Philbert Rweyemamu, alisema waliitisha mkutano huo ili kutoa maoni nini kifanyike kuendeleza sekta ya madini.

Alisema wachimbaji wa madini Tanzania wanakabiliwa na changamoto mbalimbali mojawapo ni vipengele vya sheria ya kodi kutokuwa rafiki kwa wachimbaji, ulipaji na urudishaji wa kodi.

Alisema licha ya changamoto hizo, lakini serikali imekuwa sikivu na kutatua baadhi ya changamoto, kubakiza chache ambazo kwa sasa majadiliano yanaendelea kati ya serikali na wadau kuona namna nzuri ya kufikia malengo.

# Sekta binafsi yatakiwa kuzingatia kima kipya cha chini mshahara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kupitia Idara ya Kazi, imewataka waajiri wa sekta binafsi nchini kuzingatia kima kipya cha chini cha mshahara kilichotangazwa na serikali mwaka huu kwa kuwa ni takwa la kisheria.

Kima hicho kimewekwa kwenye sekta kuu 13 ambazo ni kilimo, afya, mawasiliano, kazi za majumbani na hotelini, huduma ya ulinzi binafsi, nishati, usafirishaji, ujenzi, madini, huduma za shule binafsi, biashara na viwanda, uvuvi na huduma za baharini ili kuweka mazingira ya kazi za staha.

Akizungumza jana na kituo kimoja cha redio jijini hapa kuhusu sheria na miongozo ya kazi, Kamishna wa Kazi Msaidizi, Mahusiano kazini wa Ofisi hiyo, Andrew Mwalwisi, aliwasihi waajiri kuwalipa wafanyakazi wao kipato kulingana na kazi wanazofanya.

"Kima kilitangazwa katika tangazo la serikali 687 na kilianza kutumika Januari mosi, 2023, nisisitize kima hiki kipo katika sekta kuu 13 na nyingine ambazo hazijaanishwa, kuna kima cha chini cha kuanzia kwa kila sekta mwajiri anaweza kuanzia kwenye kima cha chini, lakini anaweza kuvuka kwenda juu zaidi sisi tumeweka hicho."

"Kuna waajiri wengine wameanza kulipa hiki kima ni kikubwa zaidi hawaruhusiwi kushusha, hiki kima cha chini ambacho walishaanza kulipa kama zaidi ya kima cha chini cha serikali, mfano sekta ya kilimo ni Sh.140,000, afya (Sh. 195,000), mawasiliano imegawanyika kuna sekta ya huduma za mawasiliano (Sh.500,000), huduma za utangazaji na vyombo vya habari, posta usafirishaji vifurushi ni (Sh. 225,000) kwa anayeanzia chini kabisa."

Alibainisha hoteli kubwa za kitalii kima cha chini ni Sh. 300,000, za kati Sh. 180,000, migahawa, nyumba za kulala wageni na baa Sh. 150,000, ulinzi binafsi (kwa kampuni kubwa Sh. 220,000 na madogo ni Sh. 148,000, sekta ya nishati (kampuni za kimataifa 592,000 na madogo ni Sh. 225,000), usafirishaji (wa anga Sh. 390,000, utoaji mizigo na usambazaji Sh. 360,000, nchi kavu kwa madereva wao wanapaswa kima cha chini kiwe Sh. 300,000 kwa mwezi.

"Kuna sekta ya ujenzi (daraja la kwanza Sh. 400,000, la pili hadi la nne Sh. 360,000, la tano hadi la saba Sh. 320,000), sekta ya madini (uchimbaji na utafutaji madini Sh. 500,000, wenye leseni za wachimbaji wadogo Sh. 300,000, biashara Sh. 450,000, madalali Sh. 250,000, huduma za shule binafsi ni Sh. 207,000, sekta ya biashara na viwanda Sh.150,000, taasisi za fedha Sh. 592,000, uvuvi na huduma ya baharini sh.238,000 na sekta nyinginezo ambazo hazijatajwa kwenye makundi hayo ni Sh. 150,000 kwa mwezi," alisema.

Alisema kima hicho kimefuta kima cha chini cha mshahara namba 196 cha mwaka 2013 na kuwataka waajiri walioajiri wafanyakazi kuzingatia kima hicho kipya.

# TMA yahadharisha 'El-Nino' mikoa 9 yatajwa kuathirika

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA), imetoa hadhari ya kuwapo kwa ongezeko la mvua nyingi (El-Nino) katika kipindi cha msimu wa vuli inayoanza Oktoba hadi Desemba, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na TMA kupitia kwa Meneja wa kituo kikuu cha utabiri, Dk. Mafuru Biseke, mamlaka hiyo imejiridhisha kupitia mifumo yake kuwa uwezekano wa kuwapo kwa El-Nino sasa ni asilimia 90.

Alisema katika utabiri wa msimu wa kipupwe ambao kawaida huanza kipindi cha mwezi Juni mpaka Agosti, waligusia kuwapo kwa ongezeko la joto kwenye eneo la bahari ya Pasifiki ambalo linalotoa viashiria vya kuwapo El-Nino.

"Wakati tunatoa utabiri wa kipupwe tuligusia kuwapo kwa hali ya joto la juu katika Bahari ya Pasifiki na tuliendelea kulifuatilia, mpaka sasa linaonekana kuongezeka zaidi na hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo kwa El-Nino na athari zake zinaweza zikaathiri baadhi ya maeneo ya nchi yetu," alisema Dk. Mafuru.

Hata hivyo, alisema mvua hiyo haitegemewi kunyesha katika kipindi hiki cha kipupwe, lakini wanazitegemea katika msimu wa vuli ambao unaanza mwezi Oktoba hadi Desemba. "Katika kipindi hiki cha kipupwe tunatarajia hali ya ukavu, upepo na baridi katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu, lakini kipindi cha vuli ndipo tunategemea mvua kubwa kwenye baadhi ya maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini mikoa ya Arusha, Tanga, Manyara na Kilimanjaro," alisema, Dk. Mafuru.

Aidha, maeneo mengine yatakayoathirika na El-Nino hiyo ni Dar es Salaam, Pwani, Zanzibar na mikoa ya Lindi na Mtwara.

"Katika utabiri wetu wa vuli ambao tunatarajia kuutoa mwishoni mwa mwezi wa nane tutatoa taarifa ya El-Nino hii kwa kuangazia mifumo yetu kuona ongezeko la joto limefikia wapi kwenye bahari ya Pasifiki," alisema Dk. Mafuru.

Alisema TMA itaendelea kufuatilia mwenendo huo na kutoa taarifa kwa wananchi kila itakapobidi ili kuwapa tahadhari ya athari ya mvua hiyo.


## Vodacom Tanzania PLC

(Imesajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)

**Taarifa ya gawio kwa mwaka ulioishia 31 Machi 2023**

Bodi ya Wakurugenzi ya Vodacom Tanzania PLC, imependekeza gawio ghafi la Shi 9.95 kwa hisa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2023. Kutokana na pendekezo hili, tafadhali zingatia tarehe zifuatazo:

- Tangazo: 20 Julai 2023
- Hisa kuuzwa pamoja na gawio: 20 Julai – 9 Agosti 2023
- Hisa kuuzwa bila gawio: kuanzia 10 Agosti 2023
- Daftari la wanahisa kufungwa: 14 Agosti 2023
- Malipo ya gawio kwa wanahisa: 16 Oktoba 2023

Wanahisa wenye mabadiliko katika taarifa zao zinazohusiana na malipo ya gawio, wanashauriwa kuwasilisha marekebisho hayo kwa msajili wa hisa ili kuwezesha malipo kwa wakati.

Msajili
CSD & Registry Company Limited
Ghorofa ya 2, Jengo la Kambarage
6 Ufukoni Street, S. L. P 70081, Dar es Salaam
Simu ya kiganjani: +255 746 160 516
Barua pepe: registrar@csdr.co.tz

**KWA IDHINI YA BODI YA WAKURUGENZI**
**Caroline Mduma**
**Katibu wa Kampuni**
**20 Julai 2023**

Pamoja tunaweza

vodacom

175061

RIPOTI YA UCHUNGUZI

## MAPENDEKEZO YA TANAPA YAKWAMA

# Mwekezaji arejesha mzigo kwa serikali

## ●Wataalamu ikolojia, uhifadhi watoa angalizo

**Na Mwandishi Wetu,** aliyekuwa BAGAMOYO

MWEKEZAJI aliyemegewa eneo katika Mbuga ya Wanyama Saadani, ameingia makubaliano mapya na serikali. Badala ya kusalimisha mita 500 kutoka ukingo wa Mto Wami, sasa atasalimisha mita 200.

Awali kulikuwa na pendekezo la kitaalamu toka Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) likitaka mwekezaji kusalimisha eneo la mita 500 kutoka ukingo wa Mto Wami ili kulinda ikolojia ya mbuga hiyo.

Katika hatua ya sasa, mwekezaji ameshikilia kusalimisha mita 200 tu kutoka ukingo wa Mto Wami na kwamba serikali ndiyo isalimishe mita 300 ili kukamilisha mita 500 zilizopendekezwa.

Kwa upande wake, serikali ilijenga hoja ya usalama na uhai wa ikolojia; kwa upande wa mwekezaji – Bagamoyo Sugar Limited (BSL) – hoja ilikuwa miwa ambayo tayari imestawishwa.

Katika vutanikuvute hii, miwa ilishinda usalama na uhai wa ikolojia. Hivyo, upande wa serikali ndio utarudi nyuma mita 300 na mwekezaji atarudi nyuma mita 200. Hayo ndiyo makubaliano.

Mwekezaji anategemea Mto Wami kupata maji kwa ajili ya kilimo cha miwa. TANAPA inategemea mto huo kwa ustawi wa wanyamapori na usalama wa ikolojia.

Janeth Msema, Msomi wa Sayansi ya Usimamizi wa Mazingira, anaonya kwamba, kilimo cha miwa kinahusisha matumizi ya mbolea na dawa kwa ajili ya kuua wadudu wanaoshambulia miwa.

Kwa hiyo, anasema mbolea na dawa hizo zinapoingia katika miili ya wanyamapori, zinakuwa na madhara kama vile kuharibu figo, ini, mfumo wa neva za fahamu, kubadili mfumo wa homoni kinga na hata kuwaua, hasa watoto wa wanyama hao ambao kinga zao hazijaimarika.

Janeth – Mhitimu wa Shahada ya Sayansi ya Usimamizi wa Mazingira kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), ana hoja nyingine kwamba, uzalishaji sukari unahusisha mitambo inayotumia mafuta na oili; hivyo huzalisha taka hatarishi ambazo zisipodhibitiwa, husababisha madhara kwa mazingira na viumbe vilivyomo.

Katika hilo, mwanamazingira huyo anafafanua kuwa, mvua inaponyesha, kemikali hizo zinaingizwa katika vyanzo vya maji na kuathiri watumiaji wa maji hayo, wakiwamo wanyamapori.

"Mnyama anapokula vitu vilivyo na, au vilivyoathirika kwa kemikali hizo; au kuzinywa katika maji, madhara yake ya moja kwa moja yanaanzia katika ini na figo. Hivi ni viungo vinavyochuja sumu mwilini. Baada ya hapo, madhara yanahamia katika mifumo ya neva za fahamu, kinga ya mwili na hata kupunguza uwezo wa wanyamapori kuzaliana.

"Kuishi kwa wanyama kunategemea kumbukumbu nzuri na hisia za kuzunguka katika mazingira yao. Uharibifu wowote katika neva zao za fahamu, kama matokeo ya uchafuzi wa mazingira kutokana na kemikali, unaweza kuwa hatari kwao.

"Miwa ni mitamu. Tembo atatamani kula miwa kwa sababu ya utamu wake. Hapo unambadilisha tembo kifikra na hisia zake katika kula. Wanyamapori wanatakiwa wale majani au nyasi za asili; siyo miwa na vitu vingine vilivyo nje ya mfumo wao wa kiikolojia," anasema.

Janeth anaendelea kufafanua kuwa wanyama wakishakula mazao yaliyozalishwa kwa kemikali na mbolea, mfumo wao wa homoni kinga unabadilika.

"Wakiugua, hawatibiki kwa dawa za kutibu wanyamapori kwa sababu hizo kemikali zinaifanya miili yao kuwa sugu kwa dawa hizo," anaonya.



Sehemu ya nyumba kwa ajili ya malazi ya wafanyakazi wa mashamba ya miwa na kiwanda cha Kampuni ya BSL wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

Uwekezaji wa kilimo cha miwa na uzalishaji sukari, anafafanua Janeth, unasababisha kelele hifadhini toka kwa wafanyakazi na ngurumo za mitambo ya kiwanda. Anasema kelele hizo ni usumbufu kwa wanyamapori.

"Ukweli mpevu ni kwamba, makosa yamefanyika kwa kutoa rukhsa ya kiwanda na kilimo cha miwa hifadhini. Kila bidhaa inayozalishwa kiwandani hapo inaweza kuathiri mazingira jirani na wanyamapori," anahitimisha Janeth, ambaye sasa anafanya kazi katika hoteli ya kitalii ya Monica kisiwani Unguja.

Hoja ya kelele inaungwa mkono na Sadick Omary, Mhitimu wa Shahada ya Sayansi ya Wanyamapori toka SUA na mtetezi wa dhati ikolojia ya mbuga za wanyama, anayesema:

"Kuna wanyama, mfano chui, hawapendi kukaa maeneo yenye kelele. Kukishakuwa na kelele hifadhini, ni usumbufu mkubwa kwao. Kama hawatohama kutoka hifadhi hiyo yenye kelele, basi kuzaliana kwao kutapungua."



Mashamba ya miwa ya Kampuni ya BSL. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

Profesa wa Mifumo na Ikolojia, Idara ya Mifumo Ikolojia na Uhifadhi ya SUA, Pantaleo Munishi, anashauri serikali izuie kilimo cha miwa na uzalishaji huo wa sukari hifadhini.

"Huo uwekezaji uondolewe kabisa katika hifadhi... Tutasababisha uhabirifu. Tungeacha kabisa kufanya kilimo na shughuli nyingine za kibinadamu ndani ya maeneo ambayo ni hifadhi za taifa.

"Sheria ya Misitu ipo. Sheria ya Wanyamapori ipo. Sheria zinazohusiana na masuala ya hifadhi za taifa na uhifadhi zipo; na zote zinazuia shughuli za aina hii kufanyika hifadhini," anasema.

Kinachoendelea Saadani kwa sasa, anasema Profesa Munishi, ni matokeo ya "watendaji wa serikali kutozingatia sheria za nchi katika utendaji wao wa kazi.

"Hawafuati sheria. Wanangoja mpaka imetokea watu wameingia hifadhini na kufanya shughuli za uharibifu, ndipo wanaanza kuja kusema aah hawa watu, eeeh...!

Anasema sheria zikifuatwa, zikazingatiwa, na kuhakikisha kuwa shughuli zote zinafanywa kwa kufuata sheria, "...hicho kinachoshuhudiwa Saadani kwa sasa (kiwanda na kilimo hifadhini) kingezuiwa, tena mapema tu!"

Profesa Munishi anakumbusha kile anachoita 'precautionary principle' (msingi wa tahadhari) – yaani kama hujui madhara ya jambo unalokusudia kulifanya, basi liache. Usilifanye!

"Kama kuna eneo tengefu ambalo limeshaingiliwa na shughuli za binadamu; hizo shughuli ziondolewe kwa sababu sheria ipo. Tufuate sheria tu. Huo ndio ushauri wangu.

"Kama hakuna uwezekano wa kuondoa shughuli hizo hifadhini, basi tutafute mbinu ambazo zinaweza kupunguza madhara, ili yasiwe tishio kubwa sana," anashauri Profesa Munishi.

Kabla ya kuzungumza na wataalamu hao, mwandishi wa habari hizi alikwenda kujionea mradi wa kilimo cha miwa na uzalishaji sukari wa kampuni ya BSL.

Alitumia dakika 28 kwa gari aina ya Toyota Coaster kutoka mjini Bagamoyo hadi Makurunge Mkwajuni, njiapanda ya Saadani, kwa nauli ya Sh. 1,500.

Kutoka hapo, kulikuwa na safari nyingine kwa pikipiki, umbali wa Km 25 iliyochukua dakika 40 hadi kiwandani kwa nauli ya Sh. 8,000. Barabara yake ni ya vumbi.

Karibu na kiwanda kuna makazi yanayoitwa, Kijiji cha Kibuyu-Mimba. Hapa pamechangamka na kuna kijiwe (kituo) cha waendesha pikipiki (bodaboda). Baadhi ya wakazi wake ni wafanyakazi wa mashamba ya miwa na kiwanda cha sukari.

Kabla ya kulifikia geti la ofisi za kiwanda hicho kutoka barabarani, kuna nyumba nane zilizojengwa kwa matofali ya saruji na kuezekwa kwa bati.

Kuna vibanda vingine vitano vilivyojengwa kwa bati kuanzia chini hadi juu. Wenyeji walisema hayo ni "malazi" ya wafanyakazi wa mradi. Karibu na nyumba hizo, kuna vibanda vitatu ambavyo mwandishi alielezwa kuwa ni vya mamalishe.

Kimsingi, mazingira ya sasa ya hifadhini Saadani, hasa katika eneo hili, yanakinzana na sheria na kanuni za nchi; na Programu ya Utalii ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya 2020-2030 inayohimiza nchi wanachama kuhakikisha kunakuwa na utalii endelevu na kuondosha vikwazo vya utalii na uhifadhi katika ukanda huo.

Tanzania ni mwanachama mwasisi wa SADC.

## Ushirikiano wa Tanzania, Ufaransa waongeza watalii

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Damas Ndumbaro, amesema ushirikiano wa Tanzania na Ufaransa umesaidia kuleta maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwamo kuongeza watalii kila mwaka nchini.

Ndumbaro aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya Siku ya Uhuru ya Ufaransa inayojulikana kwa jina la Bastille day.

Alisema Tanzania na Ufaransa zimekuwa na ushirikiano mkubwa wa muda mrefu na wamesaidia katika sekta ya kilimo, viwanda, afya, jinsia na utalii.

Pia, Ufaransa ni nchi ya pili kwa kuleta watalii wengi Tanzania ambao ni zaidi ya 100,000 kwa mwaka.

Alisema ndege ya Ufaransa imeanzisha safari za moja kwa moja kutoka Paris kuja Dar es Salaam ambayo itasaidia kuongeza ushirikiano katika sekta mbalimbali.

"Katika sekta ya nishati kuna bomba la mafuta kutoka Uganda kuja Tanzania linajengwa na kampuni ya kifaransa, hivyo mahusiano yetu ni mazuri," alisema Ndumbaro.

Kadhalika, alisema wanasherehekea siku hiyo maalum huku wakitafakari jinsi ya kuboresha mahusiano na ushirikiano kati ya Tanzania na Ufaransa.

"Mwaka 1989 Ufaransa ilifanya mapinduzi ya kuondoa utawala wa kifalme na kuweka wa kidemokrasia unaojulikana kama Bastille day ambyo ilikuwa ni magereza maarufu kule Ufaransa," alisema Ndumbaru.

Alisema wakati wanafanya mapinduzi kulikuwa na wafungwa saba na tangu Tanzania ilivyopata Uhuru wamekuwa na uhusiano mzuri na Ufaransa.

"Ndiyo maana siku ya Ufaransa kiongozi mmoja wa ngazi ya juu anaombwa kuja kuwa mgeni rasmi tukiwa tunasherehekea siku hii muhimu yapo mafanikio ya ushirikiano kati ya Tanzania na Ufaransa," alisema Ndumbaro.

Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema wamekuwa wakishirikiana na serikali kuunga mkono juhudi za Tanzania za kuleta maendeleo.

Alisema watalii wa Ufaransa sasa ni miongoni mwa mataifa mawili ya kwanza kutembelea Tanzania na kutumia bidhaa za nchini.

"Tunajivunia siku hii kila mwaka na mahusiano yetu na Serikali ya Tanzania mshikamano wetu umeleta matokeo mazuri na tutaendelea kusaidiana katika sekta mbalimbali," alisema Balozi.

Aidha, alisema wanaposherehekea siku yao maalum ni muhimu kutafakari changamoto zinazoikabili ulimwengu ikiwamo vita ya Ukraine, mabadiliko ya hali ya hewa na ukosefu wa usawa.

# Lugha yasababisha mahakama kuamuru kesi aliyehukumiwa kunyongwa kusikilizwa tena

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Kanda ya Shinyanga, imeamuru kesi ya mauaji inayomkabili, Juma Ndodi, aliyehukumiwa kunyongwa, ianze kusikilizwa upya kwa sababu hoja za awali na maelezo ya mashahidi yalisomwa kwa Lugha ya Kiswahili wakati yeye anaelewa Kisukuma.

Uamuzi huo ulitolewa juzi mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji Augustine Mwarija, Ignas Kitusi na Agnes Mgeyekwa waliosikiliza rufani iliyowasilishwa na Ndodi akipinga hatia na adhabu ya kunyongwa hadi kufa aliyopewa na Mahakama Kuu.

Jopo hilo katika uamuzi wao, walikubaliana na hoja za mawakili wa pande zote mbili kuwa mrufani alikuwa na haki kuelewa shtaka na aina ya ushahidi atakaokutana nao wakati wa usikilizwaji kesi.

"Mrufani hakuwa anaelewa lugha iliyotumiwa na mahakama, hakuna ubishi kwamba alinyimwa haki yake na hivyo hawawezi kusema kuwa mlolongo wa usomwaji wa maelezo ya mashahidi ulifanyika kwa usahihi," lilisema jopo.

Mahakama ilibainisha kwamba, mahakama ya chini haikutoa mkalimani kwa mrufani hali ambayo imemnyima haki ya kujua aina ya shtaka linalomkabili na ushahidi ambao upande wa mashtaka unatarajia kuutumia kwa maana hiyo mlolongo huo ulikuwa na dosari. "Kwa dosari zilizojitokeza tunabatilisha mlolongo wa usomwaji wa maelezo ya mashahidi wa mahakama ya chini na Mahakama Kuu, tunafuta hatia na hukumu ya Mahakama Kuu.

"Kwa minajili ya maslahi ya haki, Mahakama inaamuru kesi hiyo isikilizwe upya kuanzia hatua ya kusomwa maelezo ya mashahidi na awepo mkalimani, mrufani abaki mahabusu," lilisema jopo hilo.

Katika kesi hiyo, ilidaiwa Februari 27, 2015, Kijiji cha Buyange Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga alimuua Modester Kilijiwa.

Alisomewa shtaka lake katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama Machi 12, 2015, bila kuwapo mkalimani na Februari 3, 2016 kesi hiyo ilianza kusikilizwa Mahakama Kuu Shinyanga bila mkalimani huku yeye akiwa anaelewa lugha ya Kisukuma pekee.



Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa Airtel Tanzania, Adriana Lyamba (kushoto) na Mkuu wa Mauzo wa Benki ya Letshego Faidika, Asupya Bussi (wa pili kushoto), wakikabidhi zawadi ya bajaji kwa Peres Masige aliyeibuka kidedea katika promosheni ya Vimba na Timiza Akiba Ushinde jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni binti wa mshindi huyo, Maria Mbasha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Malalamiko ya wananchi kero mawasiliano yanafanyiwa kazi'

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema kuwa serikali inafanyika kazi malalamiko yote yanayotolewa na wananchi kuhusu huduma za mawasiliano nchini ili kuondoa kero hizo.

Aidha, miongoni mwa mipango itakayotekelezwa mwaka huu muda wowote kuanzia sasa ni kurusha satellite ya Tanzania kwa ajili ya mawasiliano.

Akifungua jana kikao kazi cha siku tatu cha viongozi wa wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape alihimiza umuhimu wa ushirikiano na upendo sehemu za kazi ili kuleta ufanisi wa kazi zao kwa haraka.

"Watanzania wanastahili huduma bora za mawasiliano na rahisi zinazopatikana kila mahali, ingawa bado kuna malalamiko ya Watanzania juu ya huduma za mawasiliano nchini. Lakini hili tunalifanyia kazi tulipatie ufumbuzi na kwa pamoja tutalimaliza," alisema.

Kuhusu uanzishwaji wa satellite kwa mwaka huu, Tanzania itafanikiwa kufikia ndoto yake ya kurusha na kuweka historia hiyo.

"Tulipokwama, tuliposuasua tutafanya tathmini ya kina na kuambiana hali ilivyo ikiwamo kufanya maboresho ili mwaka huu wa fedha 2023/24 tuweze kuendelea mbele na kutatua yote yaliokwama," alisema.

Vilevile, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa muda anaoutoa katika maboresho mbalimbali ya Wizara ya Habari na kuhudhuria shughuli mbalimbali zinazofanyika.

Alisema wizara imefanikiwa kupitia sheria, sera ikiwamo mapitio ya sheria mpya na kanuni zinazosimamia mambo mbalimbali ya habari ambazo zilikwama kwa miaka mingi.

"Tulipofanikiwa ni vizuri kupongezana na tutaagalia tuliyojipangia mwaka huu wa fedha, yapo mambo mbalimbali, lakini naamini tunaweza na tutafanikiwa, tushikamane zaidi," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohamed Khamis Abdullah, alisema wizara hiyo imepata mafaniko mbalimbali, kwa sababu ya upendo, umoja na amani walionao viongozi na watumishi.

Aliwaagiza viongozi wa taasisi mbalimbali za serikali waliopo chini ya wizara hiyo, kutumia nafasi zao za kimamlaka kwa kuwaelekeza kazi walio chini ya wizara hiyo kufanya kwa umoja, upendo na ushirikiano.

"Watumishi tukiwa na umoja na kujituma ni nguzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu yetu na ninaomba tufanye kazi kwa kujituma na si kushurutishwa, kwasababu hakuna haki bila wajibu," alisema.

Aliwaagiza wakuu wa taasisi kusimamia utekelezaji wa sera, kanuni, miongozo taratibu zinazohusu haki na utawala bora ili kuleta ufanisi zaidi za kazi zao.

Pia aliwaagiza viongozi hao kusimamia stahiki za wafanyakazi, ikiwamo utawala bora ili kila mmoja aache alama katika kazi zao.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Shomari Omari Shomari, alishukuru wizara hizo mbili za Zanzibar na Tanzania Bara kushirikiana kwa pamoja na kuahidi kuimarisha ushirikiano huo, katika kuondoa kero za Muungano ikiwamo kuongeza uchumi wa kidigitali.

Katika kikao hicho mada mbalimbali zitatolewa zikiwamo mawasiliano ndani ya taasisi, Tanzania ya Kidigitali, Mabadiliko ya Sera ya Tehama, Mpango Kazi wa shughuli za kazi, maadili ya utumishi wa umma, utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka sanjari na usalama na utunzaji wa siri za kikazi.

Pia viongozi wa taasisi hizo walipewa vitendea kazi kwa ajili ya uboreshaji wa shughuli zao za kazi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaoficha mafuta ili kulangua waadhibiwe

**IMEELEZWA** kuwapo na ulanguzi mkubwa wa mafuta ya petroli na dizeli baada ya baadhi ya wafanyabiashara kuamua kuficha mafuta hayo ili wayauze kwa bei ya juu.

Wafanyabiashara hao wanadaiwa kuyaficha mafuta hayo ili kuonekane kuna uhaba wa mafuta nchini.

Ulanguzi huo unadaiwa kukithiri kwenye mikoa inayopakana na nchi jirani na Tanzania.

Wanaotengeneza uhaba huo tunaweza kuwaita na wahujumu kwa sababu serikali inajitahidi kupunguza bei ya mafuta hayo ili wananchi wapunguziwe gharama za maisha.

Kama serikali imeamua kuchukua hatua ya kusaidia wananchi wake halafu wanakuja watu wanaotaka kujinufaisha kwa maslahi yao binafsi hao ni wahujumu.

Tumekuwa tukisikia malalamiko kutoka kwa nchi jirani kuhusu kupanda kwa gharama za maisha, huku bei ya mafuta ikiwa juu.

Katika nchi zote za Afrika Mashariki, nchi inayoongoza kwa unafuu wa bei ni Tanzania kiasi cha kuwafanya wafanyabiashara wa baadhi ya nchi hizo kuja nchini kufuata bidhaa hiyo.

Pia kutokana na gharama za maisha kupanda katika baadhi ya nchi jirani, kumesababisha kutokea machafuko ya watu kuandamana na kuharibu amani ya nchi yao.

Watu wachache wanaotaka kuharibu sifa ya Tanzania wasiachwe kuendelea kuchafua nchi na badala yake wasakwe na kuchukuliwa hatua.

Tunapongeza hatua nzuri iliyochukuliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kwa kuwaonya wanaohodhi na kulangua mafuta hayo.

Imeelezwa kuwa watu hao wanalangua mafuta hayo kwa kati ya Sh. 4,000 hadi 5,000 kwa lita ikiwa ni mara mbili ya bei elekezi.

Katika mikoa hiyo ya mipakani nan chi jirani inaelezwa kuwa uhaba umeanza kujitokeza ikiwa ni siku tano zilizopita katika miji ya Vwawa na Mlowo vituo vikidai kukosa kabisa bidhaa hiyo, huku katika mji wa mpakani wa Tunduma vituo vichache vikionekana kuuza nishati hiyo.

Bei elekezi iliyotolewa na EWURA ni Sh. 2,853 kwa petroli na Sh. 2,660 kwa dizeli kwa Mkoa wa Songwe.

Juzi EWURA ilitoa taarifa ya onyo kwa baadhi ya kampuni za mafuta zinazohodhi mafuta wakisubiri mabadiliko ya bei.


Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, ilisema walipokea taarifa za uwapo wa baadhi ya kampuni za mafuta kuhodhi mafuta kwa ajili ya maslahi binafsi ya kibiashara ikiwamo kusubiri mabadiliko ya bei.

Pia, ilibaini kuwapo kampuni nyingine zinazodaiwa kupakia mafuta kutoka kwenye maghala bila kuyauza na nyingine kukataa kuuza mafuta hayo kwa wamiliki wa vituo wasio kuwa na ubia au mikataba nao.

EWURA ilisema mpaka Julai 14, mwaka huu, mafuta yote yaliyokuwapo nchini ni lita 169,853,692 za petroli, lita 209,641,670 za dizeli, na lita 34,588,002 za nafuta ya ndege yanayotosheleza mahitaji.

Kampuni za mafuta zinazohodhi mafuta zimeonywa na kutakiwa kuacha mara moja, kufanya hivyo ni kinyume cha sheria, kanuni zinazosimamia biashara ya mafuta nchini na masharti ya leseni zao za biashara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Acheni kuongeza ugumu kudhibiti dawa za kulevya

**MATUMIZI** ya dawa za kulevya, yamechangia kuangamiza nguvukazi ya taifa ambayo wengi ni vijana, kutokana na sehemu kubwa hujihusisha na kutumia vilevi hivyo hatarishi.

Wanaotumia dawa wanaharibikiwa kimaisha, huku baadhi wakiiba vitu kutoka nyumbani kwao na kuviuza, wapate pesa za kununulia dawa hizo, hali inayowafanya wengine kutengwa na jamii lakini hata kuumizwa au kuuawa kwa tuhuma za wizi na udokozi.

Juhudi mbalimbali zinafanyika ili kudhibiti matumizi hasa kuzuia uingizwaji wa dawa hizo, kujenga nyumba kwa ajili ya kuhifadhi waraibu, kuanzisha vituo vya kutolea dawa za methadone, kwa ajili ya waraibu, ambao huzitumia ili kuondoa hamu na tamaa waweze kurudia katika maisha yao ya zamani kabla ya kuingia huko.

Wakati juhudi hizo zikifanyika, kuna madai ya kuwapo mbinu chafu za kusababisha waraibu waendelee kuwapo, zinazofanywa na baadhi ya watu, lakini Rais Samia Suluhu Hassan amezishtukia na kutoa onyo kwa wahusika

Rais anazionya gereji zinazofanya biashara ya unga unaotoka katika masega ya gari yaitwayo (catalytic converter), kwa ajili ya kutengeneza dawa za kulevya hizo.

Kwa mujibu wa Rais, wanachukua huo unga kwenye magari wanakwenda kuchanganya na dawa za kulevya, na kwamba ndio sababu watumiaji wa dawa hizo wanafariki ghafla.

Aatoa onyo hilo, Juni 25, 2023 mwaka huu, katika maadhimisho ya kitaifa ya kupiga vita matumizi na biashara ya dawa za kulevya duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Arusha.

Ninaamini kwamba onyo hilo la Rais likizingatiwa, matumizi au biashara ya dawa inaweza kudhibitiwa na kulifanya taifa la kesho kuwa salama dhidi ya matumizi ya dawa hizo hatari.

Ikumbukwe, mwaka jana, waraibu 871,010 walinufaika na tiba, huku 245 kati yao waliopata nafuu wakiunganishwa na vyuo vya ufundi ili wapate ujuzi wa kujiajiri wasirejee katika matumizi ya dawa za kulevya.

Takwimu hizo, kwa mujibu wa Waziri wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, ambaye anasema serikali imeongeza kasi ya kukabiliana na matumizi ya dawa hizo.

Lakini pia, hatua hizo zinazochukuliwa na serikali, zinahusisha kodi za wananchi, hivyo wanaofanya biashara au matumizi yake, wangeacha ili serikali iokoe pesa na kuzipeleka kwenye matumizi mengine ya muhimu.

Pesa haziishii hapo tu bali pia ujengaji wa kwa ajili ya waraibu (sober houses), nao unahitaji fedha, dawa za methadone nazo zinahitaji pesa, hivyo njia ya kuziokoa ni wahusika kuachana mfumo huo wa maisha.

Baadhi ya waraibu wamekuwa wakidai kwamba kuacha uraibu ni vigumu. Binafsi sina uzoefu wake, lakini pia ingekuwa vyema mtu kutafakari kwa umakini hatima ya maisha yake na kuamua kuacha.

Mratibu akiacha atakuwa ameokoa afya yake, lakini na pesa za walipa kodi ili zielekezwe kwenye huduma nyingine badala ya kung'ang'ania maisha ambayo hatimaye yake ni mbaya.

Inasikitisha kuona baadhi ya waraibu wakipelekwa kwenye nyumba za kuwatunzia lakini baadaye wanatoroka na kurudi mitaani kuendelea na maisha ya uraibu bila kujali kwamba wanajihatarisha.

Lakini pia kama ingewezekana, basi nyumba hizo zingejengwa za kutosha, kwani katika maeneo mengi waraibu hufika vituo vya kutolea dawa za methadone na kunywa kisha wanarydu nyumbani.

Ukweli kwamba baada ya kunywa methadone na kurudi katika mazingira ambayo yalisababisha akawa mraibu, ni rahisi kushawishika na kuendelea kutumia dawa hizo hata kama ameamua kuacha, hivyo uwapo wa nyumba za kutosha za kuwatunzia ninadhani ni jambo muhimu.

# TAARIFA YA VIWANGO VYA TIGO KWA ROBO YA PILI (APRILI - JUNI 2023)

## Viwango unavyotozwa kwa kadri unavyotumia (Na Kodi)

** - Malipo ya sauti yamekadiriwa kwenye sekunde iliyo karibu
- Malipo ya data yamekadiriwa kwa shilingi 0.09 kwa kila kilobaiti 10 za data

### VIWANGO VYA NDANI

| Aina za simu | Bei (TSh/Dk) |
|---|---|
| Tigo - Tigo (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |
| Tigo - Mitandao mingine (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |

### VIWANGO VYA KIMATAIFA - TIGO

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 720 | China, India, Marekani, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Angola, Afrika Kusini, Nigeria, Botswana, Ghana, Ethiopia |
| Kundi 3 | 1020 | Lebanon, Israeli, Hispania, Falme za Kiarabu, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani) |
| Kundi 4 | 1200 | Sweden, Hong Kong, Pakistani, Yemen, Ufilipino, Saudi Arabia, Uholanzi, Japan, Malaysia, Norway, Ireland, |
| Kundi 5 | 1800 | Australia, Nepal, Uturuki, Urusi, Visiwa vya Comoro, Uganda, Rwanda, Ufaransa, Denmark, Italia, Oman, Ujerumani |
| Kundi 6 | 2520 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 7 | 2520 | Cuba, DRC, Burundi, Zimbabwe, Msumbiji, Uswisi, Malawi, Zambia |
| Kundi 8 | 19800 | Mitandao yote ya satelaiti |

### VIWANGO VYA KIMATAIFA - ZANTEL

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 497 | Marekani, India, China, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Falme za Kiarabu, Afrika Kusini, Denmark, Sweden, Norway, Ireland, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani), Hispania, Ufaransa, Italia, Pakistan, Zimbabwe, Ujerumani |
| Kundi 3 | 1325 | DRC, Yemen, Omani, Lebanon, Israel, Sudani |
| Kundi 4 | 1500 | Zimbabwe (simu za kiganjani), Msumbiji, Malawi, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia, Mayote, Sudani ya Kusini |
| Kundi 5 | 1200 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 6 | 3000 | Cuba, Vanuatu, Tunisia, Tonga (simu za kiganjani), Tokelau, Uswisi, Somalia,Visiwa vya Shelisheli, Nauru, Samoa, Madagascar, Slovenia, Visiwa vya Comoro |
| Special | 18000 | Mitandao yote ya satelaiti |

### VIWANGO VYA SMS

| Aina za SMS | Bei (TSh/SMS) |
|---|---|
| SMS za kitaifa | 8 |
| SMS za kimataifa | 215 |

### VIWANGO VYA DATA

| Intaneti | Bei (TSh) |
|---|---|
| Data kwa MB | 9.35 |

## VIWANGO VYA VIFURUSHI VYA DAKIKA, INTANETI NA SMS (Na Kodi)

### MITANDAO YOTE

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 500 | 90 | 10 | 100 | 25 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 0 | 30 | 30 | 25 | 10 | Saa 24 |
| 1000 | 0 | 150 | 150 | 25 | 0 | Saa 48 |
| 1500 | 250 | 50 | 300 | 30 | 0 | Siku 7 |
| 2000 | 0 | 250 | 250 | 100 | 50 | Siku 7 |
| 3000 | 0 | 400 | 400 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 3000 | 55 | 70 | 125 | 50 | 1024 | Siku 7 |
| 5000 | 100 | 180 | 280 | 100 | 1434 | Siku 7 |
| 5000 | 0 | 300 | 300 | 50 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 0 | 1200 | 1200 | 50 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 0 | 500 | 500 | 50 | 3072 | Siku 30 |
| 20000 | 0 | 800 | 800 | 50 | 7168 | Siku 30 |
| 30000 | 0 | 900 | 900 | 500 | 11264 | Siku 30 |

### SMS

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 200 | 0 | 0 | 0 | 200 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 0 | 0 | 0 | 1000 | 0 | Siku 7 |
| 1000 | 0 | 0 | 0 | 10000 | 0 | Siku 30 |

### BILA KIKOMO

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1000 | 0 | 30 | 30 | 50 | 0 | Bila Kikomo |
| 1000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 250 | Bila Kikomo |

### INTANETI

| Bei (TSh) | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 500 | 246 | 24 hrs | N/A |
| 1000 | 492 | 24 hrs | N/A |
| 2000 | 985 | 24 hrs | N/A |
| 2000 | 950 | 7 days | N/A |
| 2100 | 1024 | 7 days | N/A |
| 3000 | 1434 | 7 days | N/A |
| 5000 | 2458 | 7 days | N/A |
| 10000 | 4915 | 7 days | N/A |
| 15000 | 7373 | 7 days | N/A |
| 10000 | 4608 | 30 days | N/A |
| 20000 | 9830 | 30 days | N/A |
| 35000 | 17203 | 30 days | N/A |
| 50000 | 24576 | 60 days | N/A |
| 75000 | 34816 | 60 days | N/A |
| 100000 | 49152 | 60 days | N/A |

### KIMATAIFA - TIGO

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 10 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 40 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Nigeria,Ghana - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Misri - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 4 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 80 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Nigeria,Ghana - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Misri - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Algeria, Morocco, Tunisia - Dk 5 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 12 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Nigeria,Ghana - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Misri - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 180 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 18 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Ufaransa - Dk 13 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Nigeria, Ghana - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Misri - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 24 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Oman, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 38 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Algeria, Morocco, Tunisia - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |

### KIMATAIFA - ZANTEL

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | China, India - Dk 22 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Afrika Kusini, Mauritius - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon, Yemen, Sudan, Misri - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Oman - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Ufaransa - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Ujerumani, Italia, Uingereza (simu za mezani), Uturuki - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Uganda, Rwanda - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Afrika Kusini, Mauritius - Dk 11 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon, Yemen, Sudan, Misri - Dk 11 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Oman - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | China, India - Dk 110 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 7500 | Ujerumani, Italia, Uingereza (simu za mezani), Uturuki - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 7500 | Kenya, Uganda, Rwanda - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |

**MIC TANZANIA PLC,**
Derm Complex, Kiwanja Namba 11, Kitalu 45 A, Barabara ya Bagamoyo
S.L.P. 2929, Dar es Salaam, Tanzania.

**www.tigo.co.tz**

217504902

# Mkenda amulika ubora wa vyuo vikuu

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameitaka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kuongeza jitihada katika udhibiti wa ubora wa vyuo vikuu ili kuhakikisha azma ya kuwa na mitaala inayojibu mahitaji ya soko na ajira inatimia.

Vilevile, amezitaka taasisi za elimu ya juu kuendelea na mapitio ya mitaala iliyopo kwa kuzingatia miongozo iliyopo ili kuendana na mabadiliko ya soko la ajira na mahitaji ya sasa ya kiuchumi na kijamii.

Prof. Mkenda alielekeza hayo juzi alipofungua Maonesho ya 18 ya Vyuo Vikuu yaliyoanza Jumatatu na kuhudhuriwa na taasisi za vyuo vikuu 83 vya ndani na nje ya nchi.

Maonesho hayo ambayo yamebebwa na kaulimbiu ya 'Kukuza ujuzi nchini kupitia elimu ya juu sayansi na teknolojia kwa uchumi imara na shindani', yanatarajia kufungwa Jumamosi.

Akizungumza katika uzinduzi huo, waziri huyo aliitaka TCU iongeze jitihada katika masuala ya utafiti na kusimamia vyuo vikuu ili kuvifanya kuwa chachu ya maendeleo na suluhisho la changamoto mbalimbali za maendeleo ya jamii na taifa.

Waziri Mkenda alisema amefurahi kuona washiriki wa maonesho hayo baadhi wametoka nje ya nchi zikiwamo taasisi ambazo zinasaidia vijana kwenda kusoma huko.

Prof. Mkenda alizitaka taasisi za elimu ya juu zihakikishe zinabuni na kuanzisha programu mpya zinazokwenda na wakati.

Pia alizitaka ziimarishe au kuanzisha ushirikiano wenye tija na taasisi za utafiti na maendeleo pamoja na sekta binafsi hususani viwanda na kuweka utaratibu wa kuendeleza teknolojia zinazozalishwa na kuhamasisha matumizi yake ili kuongeza kasi ya maendeleo.

Akizungumzia kaulimbiu ya mwaka huu ya maonesho hayo, kiongozi huyo alisema inaakisi hali halisi na matarajio ya Watanzania hususani wakati huu ambao taifa linaendelea na mchakato wa mapitio na mageuzi ya elimu.

Waziri huyo alisema mwaka 1961, nchi ilikuwa na chuo kikuu kishiriki kimoja yaani Chuo Kikuu kishiriki cha Dar es Salaam ambacho kilikuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha London, kikiwa na wanafunzi 14 tu lakini hadi kufikia 2023, kuna jumla ya vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki 49. Kati yake, vyuo vikuu kamili ni 32 na vishiriki ni 17.

Alisema kati ya hivyo, vyuo 19 vinamilikiwa na serikali na 30 vinamilikiwa na sekta binafsi na kwamba, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi 14 mwaka 1961 hadi wanafunzi 314,643 mwezi Mei mwaka huu.

Kwa upande wa ufadhili na ugharamiaji wa elimu ya juu, kiongozi huyo alisema serikali imeongeza wigo wa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELSB), ufadhili wa Samia pamoja na mikopo inayotolewa na taasisi za fedha.

Prof. Mkenda alisema ndani ya miaka mitano ijayo, serikali imepanga kuweka njia bora ya kuharakisha utekelezaji na uimarishaji wa taasisi za ubunifu na utafiti kwa lengo la kutoa suluhisho la changamoto za wakulima, wenye viwanda na watumiaji wengine wa teknolojia.

Waziri Mkenda alisema Taasisi ya Teknolojia ya India imeanzisha kampasi yake Zanzibar na inatarajia kuanzia mwezi Oktoba kuanza udahili wa wanafunzi na watafundisha kwa viwango vilevile walivyonavyo nchini humo.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema kati ya taasisi 83 zilizoshiriki maonesho hayo, zipo zilizoshiriki zenyewe kutoka nchi ya Kenya na India na nyingine zaidi ya 20 zilizoshiriki kupitia mawakala wanaopeleka wanafunzi nje ya nchi.

Alisema taasisi zilizoshiriki zinajumuisha 64 zinazotoa mafunzo kwa ngazi ya elimu ya juu, Umoja wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu (TAHLISO), wakala wa vyuo vikuu vya nje (tisa) na taasisi zingine mbalimbali zikiwamo za serikali.



Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo (kushoto), akizungumza katika uzinduzi wa SimBanking App inayotumia teknolojia ya kisasa zaidi inayowezesha kutambua mahitaji ya wateja na kurahisisha huduma na miamala jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yazindua mfumo mpya huduma za kibenki kwa simu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI dunia ikishuhudia mabadiliko makubwa ya teknolojia yanayochagiza maendeleo katika nyanja mbalimbali za maisha, Benki ya CRDB imezindua mfumo mpya wa kupata huduma za kibenki kwa kutumia simu (SimBanking App) inayotumia teknolojia ya kisasa ili kutambua mahitaji ya wateja.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa programu hiyo jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo, alisema mfumo huo mpya umetengenezwa kwa muunganiko wa teknolojia za kisasa ikiwamo akili bandia (artificial intelligence).

"Teknolojia iliyotumika katika SimBanking App hii inampa uwezo mteja kuchagua mpangilio wa huduma kwa namna ambavyo yeye mwenyewe angependelea, teknolojia hiyo pia ina uwezo wa kutambua ni huduma gani mteja anapendelea zaidi na kumrahisishia namna ya kuipata," alisema.

Nshekanabo alibainisha kuwa teknolojia hiyo mpya ni ya kimapinduzi katika kufikisha huduma za fedha kwa wateja kwa kuwa itaongeza wigo wa huduma zinazoweza kutolewa kidijiti huku kasi ya miamala ya wateja ikirahisishwa kwa kiasi kikubwa.

"Eneo lingine ambalo tumelipa uzito mkubwa katika SimBanking App hii mpya ni ulinzi na usalama wa taarifa na miamala ya wateja. Tunatumia teknolojia ya baiometriki kuhakikisha usalama kwa wateja. Hii inatufanya kuwa benki pekee nchini na kati ya chache barani Afrika inayotumia teknolojia hii," aliongezea Nshekanabo.

Akizungumzia huduma mpya ambazo zimeongezwa, Meneja Mwandamizi wa Huduma za Kidijiti na Ubunifu wa Benki ya CRDB, Jacklina Jackson, alisema SimBanking App inatoa fursa za uwekezaji kwa wateja kwa kuwawezesha kuwekeza kupitia akaunti za uwekezaji (Fixed Deposit) kidijiti.

"Wateja pia sasa hivi wanaweza kupanga uhamisho wa fedha na malipo yanayojirudia au ya mara kwa mara kwa urahisi. Uhamisho unaweza kupangwa kila siku, kila wiki au kila mwezi. Tumeboresha upande wa kumbukumbu za taarifa za miamala ambapo wateja wanaweza kupata risiti ya miamala yote wakati wowote kwa urahisi," alisema Jacklina.

Katika upande wa malipo, alisema SimBanking App imeboresha malipo kupitia watoa huduma za kidijiti kwa kuwezesha ukusanyaji wa malipo kupitia programu hiyo ambapo mteja ana uwezo wa kutoa rukhsa ya malipo kwa kutumia mfumo wa namba ya siri ya mara moja (one time passcode).

"Vilevile, tumefanya maboresho katika huduma za bima kwa kuongeza kasi na muda wa upatikanaji wa huduma," aliongezea Jacklina kuhusu huduma hiyo ya bima za vyombo vya moto ambayo ilizinduliwa kwa mara ya kwanza kupitia SimBanking App mwaka 2020 benki hiyo ilipofanya maboresho.

Kupitia mfumo huo mpya, benki hiyo pia inakuja na programu ya uaminifu (loyalty program) inayowawezesha wateja kupata alama wanapotumia mfumo kisha kujishindia zawadi. Pia kutoa maoni yao kila wakati wanapokamilisha miamala.

Hii ni mara ya pili kwa Benki ya CRDB kufanya maboresho makubwa katika huduma ya SimBanking baada ya maboresho yaliyofanyika mwaka 2020. Tarifa ya benki hiyo inaonyesha kwq sasa asilimia 96 ya miamala yote inafanyika kidijitali huku SimBanking ikichangia sehemu kubwa.

# Auawa kwa kuchomwa moto tuhuma za wizi

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANANCHI waliotajwa wenye hasira Manispaa ya Lindi mkoani hapa, wamemuua kwa kumchoma moto kijana ambaye jina na mahali anakoishi hakujafahamika, baada ya kudaiwa kuiba vyombo vyenye thamani ya Sh. 85,000 nyumbani kwa Pilli Ally.

Tukio la kuuawa kijana huyo mwenye umri unaokadiriwa kuwa kati ya 30 na 32 limethibitishwa na mamlaka husika. Lilitokea Julai 14, mwaka huu katika Mtaa wa Mangomboli mjini Lindi.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo wamedai kuwa siku hiyo, mtuhumiwa kabla ya kukutwa na umauti, aliingia ndani ya nyumba ya mama huyo kisha kuiba fedha na vyombo vya kupakulia vyakula (ho pots) wakati mmiliki huyo akiwa amekwenda bombani kuteka maji.

Walidai kuwa wakati kijana huyo akiwa anatoka ndani ya nyumba hiyo, alikutana na mama mlangoni kisha kumsukuma na kudondoka chini na kukimbilia nje, jambo ambalo lilimfanya Pili apige kelele kuomba msaada wa wananchi wenzake walijitokeza na kumshushia kipigo kijana huyo.

"Huyu mama wakati anarejea alimkuta mwizi anatoka ndani mkononi akiwa ameshikilia poti akitoka nje na kusukumwa na kudondoka chini, akapiga kelele za mwizi," walidai Daudi Mbuyu na Happy John, wakazi wa eneo hilo.

Pili ambaye ni mmiliki wa nyumba hiyo, akizungumza kabla ya askari kuwasili eneo la tukio, alidai kijana huyo alimkuta ameibia fedha taslimu Sh. 85,000, vyombo vitatu vya kuwekea chakula na redio moja.

Alisema ni mara ya pili kwake kumkuta kijana huyo akiwa ndani ya nyumba yake akiwa anamwibia, lakini alikuwa anazidiwa nguvu na kibaka huyo kwa kumsukuma na kudondoka chini na kutoa nafasi ya kutokea nje na kukimbia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Pili Mande, alithibitisha kutokea mauaji ya kijana huyo asiyefahamika jina wala mahali anakoishi na kueleza mwili wa mtuhumiwa huyo umepelekwa kuhifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi (Sokoine) mjini Lindi, ukisubiri ndugu na jamaa wautambue na kuchukua kwa ajili ya mazishi.

Mande alitoa rai kwa wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mikononi mwao kwa kuwa kama kijana huyo ni kibaka, angelisaidia Jeshi la Polisi kuwataja wenzake wanaoshirikiana nao katika vitendo hivyo.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Alexander Makalla, pia alithibitisha kupokewa mwili wa kijana huyo hospitalini huko, ukipelekwa na askari wa Jeshi la Polisi.

Dk. Makalla aliwaomba ndugu kufika hospitalini huko kuchukua mwili wa kijana huyo kwa ajili ya maziko.

## Zahanati ya Polisi Manyara yahudumia wananchi 34,530

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANANCHI 34,530 wametajwa kuhudumiwa na Zahanati ya Jeshi la Polisi mkoani Manyara kila mwezi na kusaidia kutatua tatizo la kufuata umbali mrefu huduma za afya.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Lucas Mwakatundu, wakati akisoma taarifa ya ujenzi wa Zahanati ya Polisi katika Kata ya Bagara wilayani Babati mbele ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni.

Mwakatundu alisema kwa mwezi wanawahudumia watoto chini ya miaka mitano 440, wajawazito 33, wanachama wa Bima ya CHIF 410, wanachama wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) 320 na wagonjwa wanaolipia 360.

Awali alisema mradi huo ulianza kujengwa mwaka 2013 chini ya ufadhili wa Shirika la PharmAccess International ambapo ilitoa Sh. mil. 51.2, uchangiaji wa wananchi Sh. mil. 30.6 na serikali ilitoa Sh. mil. 54. Aidha, alimweleza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa kikwazo walichonacho ni upungufu wa wafanyakazi hasa kitengo cha maabara.

Naye Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, baada ya kuzindua zahanati hiyo alisema serikali imeboresha huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya mpaka hospitali za rufani za mikoa ambapo kuna vifaa vya kisasa tofauti na zamani.

Masauni alisema lengo la serikali ni wananchi wapate huduma bora huku akidai kuwa fedha zilizotolewa na mataifa mbalimbali kusaidia mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona zimesaidia sana kuimarisha huduma za afya.

Mkazi wa Kijiji cha Nakwa, John Bura alisema huduma zinazotolewa na zahanati hiyo ni nzuri licha ya kuwa ilikuwa haijazinduliwa.

Aliomba serikali kuimarisha huduma zote za watoto wachanga ili kuwaepusha na magonjwa mbalimbali.

# Naibu Waziri akemea unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na VVU

**Na Mary Mosha,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, amekemea unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), huku akieleleza ni lazima wajumuishwe katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Ummy alieleza masikitiko yake hayo jana, alipokuwa akikagua utekelezaji wa shughuli za watu wanaoishi na virusi hivyo katika Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Umefika wakati jamii kuacha tabia za unyanyapaa jina na badala yake kuwa shirikishi katika shughuli za kijamii ili waweze kujipatia mahitaji muhimu na kuendelea kutumia dawa.

"Tuache unyanyapaa kwa WAVIU (Wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi), tusiwabague, tuishi nao kama watu wengine. Tuwapende na tujenge tabia ya kuwathamini, kujali na kuwajumuisha katika masuala mbalimbali ya uzalishaji," alisema.

Aidha, aliwakumbusha vijana wanaoishi na maambukizi hayo kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na Halmashauri ya Manispaa na Wilaya ili kujiongezea mitaji na kujikwamua kiuchumi.

"Vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35 bado wanategemea na taifa katika uzalishaji wa shughuli za maendeleo. Hivyo, acheni mienendo isiyo faa, zingatieni dawa na walimisheni wenzetu ili wasije kuambukizwa, nyinyi ni taifa la leo na kesho, hatutegemei kuona maambukizi ya kiongezeka," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema kazi kubwa inayofanywa hivi sasa na serikali mkoani humo ni kuendelea jitihada mbalimbaili za kuhakikisha maambukizi mapya yanadhibitiwa.

"Pamoja na jitihada za serikali katika mapambano haya, bado vijana mnakazi kubwa ya kuendelea kujilinda kwa njia zote muhimu zinazoshauriwa na wataalam wa afya huku mkikumbuka kuachana na tabia zote hatarishi zinazoweza kuchochea mtu kupata maambukizi haya," alieleza Babu. Awali, Mratibu wa Ukimwi, Mkoa wa Kilimanjaro, Jesca Nyaki, alisema kiwango cha maambukizi kimeendelea kupungua kutoka asilimia 7.3 mwaka 2003/24 hadi kufikia asilimia 2.6 mwaka 2016/17.

Naye Mwenyekiti wa Konga ya Moshi Vijijini, Baltazar Minishi, aliishukuru serikali kwa uwezeshwaji na huduma za afya wanazozipata kutoka serikalini kwani zimeboreshwa na kuleta tija kwa WAVIU.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Muheza mkoani Tanga, Benard Luanda (wa tatu kulia), akiwafundisha wanafunzi wa darasa la sita namna ya umwagiliaji bora bustani ya miti kwa ajili ya kutunza mazingira shuleni hapo, juzi. Kushoto ni Mwalimu Msaidizi, Selijo Mwihava. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanafunzi wenye ulemavu wapewa viti mwendo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WANAFUNZI 17 wenye ulemavu wa viungo katika shule za msingi na awali katika Halmashauri ya Arusha iliyoko Wilaya ya Arumeru, wamepatiwa msaada wa viti mwendo 17.

Msaada huo umetolewa na shirika lisilokuwa la kiserikali la CCBRT Kanda ya Moshi na kukabidhiwa kwa uongozi wa halmashauri hiyo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi hao.

Akizungumza jana, wakati wa kukabidhi kwa viti mwendo hivyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Ojung'u Salekwa, amewashukuru wadau wa Shirika la CCBRT kwa msaada huo muhimu na wathamani kwa watoto wenye ulemavu.

Alisema licha ya watoto hao kuwa na changamoto lakini wazazi wenye watoto wenye ulemavu wanapitia matatizo mengi zaidi hasa katika malezi.

Pia alisema kuna umuhimu kwa jamii kuungana na kutoa msaada wa hali na mali pamoja na kuwatia moyo familia zenye watoto hao.

"Tunalo jukumu kubwa la kuwahudumia watoto wenye ulemavu, kila mtu anayo nafasi ya kufanya jambo kwa familia hizi kwa kuwa tatizo la malezi ya watoto hawa ni zaidi ya maisha ya kawaida ya binadamu, tutumie muda hata kuwatia moyo," alisema Mwenyekiti huyo.

Aidha aliipongeza serikali kwa kuweka mazingira bora kwa wadau wa maendeleo kwa kuwa inathamini kazi kubwa inayofanya na wadau na aliwataka kuendelea kuisaidia serikali katika kuhudumia jamii hasa watoto wenye mahitaji maalumu.

Mratibu wa Huduma za Viti Mwendo kutoka CCBRT, Neophita Lukiringa, alisema lengo la shirika hilo ni kutoa msaada huo ni kuwasaidia watoto kuweza kwenda shuleni na kufanikisha ndoto zao za kielimu, pia kuwasaidia wazazi kurahisisha kazi ya kuwahudumia watoto hao.

Hata hivyo, wazazi na watoto waliopewa viti hivyo, wameshukuru kwa msaada huo ambao wamekiri ni huduma kwa kuwa walemavu wengi wanaihitaji kwa ajili ya kutoka sehemu moja kwenda nyingine.


Fatuma Yusuph, mama wa Sahil Yusuph mtoto mwenye umri wa miaka tisa, ameshukuru kwa msaada huo, huku akiiomba jamii kuendelea kuwasaidia wazazi wenye watoto wenye mahitaji maalumu kwa kuwa malezi ya watoto hayo yana gharama kubwa na yanahitaji mzazi kutumia muda mwingi bila kufanya shughuli nyingine za uzalishaji.

"Mtoto wangu ana miaka tisa sasa, nahitajika muda wote kuwa nae karibu, ili kumuhudumia akiwa na kiti mwendo itanipunguzia kidogo kazi na mimi kupata muda wa kufanya majukumu mengine," alisema Fatuma.

Naye Rachel Mollel, mtoto aliyepewa kiti alimshukuru serikali kwa msaada huo, kwa kuwa kitamsaidia kutembea akiwa shuleni na nyumbani pia.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Selema Msumi, alishukuru kwa msaada huo, alisema kuwa halmashauri ina watoto 509 wenye uhitaji wanasoma kwenye shule zenye vitengo maalumu, huku watoto 77 wakisoma kwenye Shule ya Bweni ya Ilboru hivyo mahitaji ya watoto hao ni mengi kulingana na idadi yao.

Awali uongozi huo licha ya kuwashukuru wadau unawaomba wadau kuendelea kujitokeza kuchangia maendeleo ya jamii katika halmashauri hiyo.



# Vyombo vya habari vyapewa 5 utoaji elimu matumizi mbolea

**Na Timothy Itembe,**
MARA

CHAMA cha Ushirika cha Wakulima Mkoa wa Mara (WAMACU) kimevipongeza vyombo vya habari mkoani hapa kutokana na juhudi za kuhamasisha ununuzi na matumizi sahihi ya mbolea ya ruzuku hali iliyosababisha kupungua kwa wizi wa mbolea hiyo.

Inaelezwa kuwa awali mbolea hiyo ilikuwa ikisafirishwa kuelekea Kenya kinyemera na kuuzwa kimagendo lakini baada ya vyombo vya habari kupaza sauti tabia hiyo imepungua.

Pongezi hizo zimetolewa juzi na Meneja Mkuu wa WAMACU, Samwel Marwa, mbele ya Bodi ya Kampuni ya Mbolea TFRA iliyofika wilayani Tarime kwa lengo la kujifunza mafanikio ya kufanya vizuri katika usambazaji wa mbolea kwa wakulima kwa msimu wa mwaka 2022-2023.

"Katika msimu wa 2022-2023 WAMACU kwa kushirikiana na TFRA pamoja na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) ilisambaza mbolea zaidi ya tani 198 kwa wakulima wa wilaya za Tarime, Rorya na Butiama na hili limefanikiwa kutokana na msaada wa vyombo vya habari," alisema Bisiboye.

Kadhalika, alieleza kuwa kwa WAMACU mbolea imekuwa fursa kwa kukiongezea chama mapato hasa baada ya kuanza kusambaza mbolea ya Kampuni ya OCP ambao walitoa kamisheni ya Sh.5,000 kwa kila mfuko wa kilogramu 50.

Mwenyekiti wa WAMACU, David Hechei alisema chama kinaendelea kutumia vyombo vya habari kama vile redio, television, magazeti na mitandao ya kijamii katika kuhamasisha ununuzi na utumiaji wa mbolea ya ruzuku ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Athony Diallo alisema walifika katika chama hicho lengo likiwa ni kujifunza juu ya mafanikio yenye tija katika usambazaji wa mbolea ya ruzuku mkoani humo.

Meneja TFRA Kanda ya Ziwa, Dk. Asheri Kalala alipongeza WAMACU kusambaza mbolea ya ruzuku kwa ubora licha ya kuwa ni muda mfupi wameanza shuguli hiyo lakini mafanikio yameonekana, hivyo kuwataka kuendeleza juhudi hizo katika kufikia mafanikio.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja (katikati), akikagua maendeleo ya ujenzi wa chanzo cha maji cha mradi wa maji wa Tarime-Rorya juzi, ambao unajengwa kwenye chanzo cha Ziwa Victoria na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 29 za maji kwa siku. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwenge wa Uhuru kuzindua miradi 42 Shinyanga

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amesema kuwa Mwenge wa Uhuru unatarajia kuwasili mkoani hapa, kwamba utakagua na kuzindua miradi ya maendeleo 42 yenye thamani ya Sh.bilioni 13.4.

Alisema Mwenge wa Uhuru utawasili Julai 27 mwaka huu na kukimbizwa katika halmashauri sita za mkoa huo, ambazo ni Kishapu, Shinyanga, Ushetu, Msalala, Manispaa ya Kahama na Shinyanga.

Mndeme alibainisha hayo juzi wakati akikagua miradi ya maendeleo ambayo itapitiwa na Mwenge huo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Manispaa ya Kahama na kueleza kuridhishwa na utekelezaji wake pamoja na maandalizi ya kupokea.

"Nimetembelea miradi ya elimu, afya, mazingira, kilimo, miundombinu na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Miradi yote ni mizuri na ziara hii ni endelevu katika halmashauri zote, lengo ni kuhakikisha miradi yote itakayotembelewa haina kasoro," alisema Mndeme.

Aidha, aliwaomba wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kujitokeza kwa wingi kuupokea mwenge huo ambapo utakuwa ukipita katika maeneo yao pamoja na kuwazindulia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Naye Mratibu wa sherehe za Mwenge wa Uhuru Manispaa ya Kahama, Sadick Kigaile, aliitaja miradi ya maendeleo ambayo itapitiwa ni miradi ya kilimo, shamba la miti, ofisi ya Kata Nyihongo, jengo la maabara katika Hospitali ya Wilaya Kahama, miundombinu ya barabara na uzinduzi wa Jukwaa la Wanawake Kiuchumi na Shule ya Sekondari kagongwa.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga miradi ambayo itapitiwa ni kikundi cha vijana wabunifu Kata ya Busanda, mashine ya kukoboa nafaka na kuongeza thamani ya mazao Kata ya Didia na kikundi cha ufugaji nyuki pamoja na miradi ya elimu na afya.

# Serikali yatoa mil.603/- ujenzi sekondari mpya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imetoa Sh. milioni 603.8 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Kijiji cha Ngilimba.

Hatua hiyo itawasaidia wanafunzi zaidi ya 400 wa Shule ya Sekondari Ulowa iliyopo katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga ambao kwa sasa wanalazimika kutembea kilometa 15 kuifuata shule hiyo.

Wanafunzi hao ni kutoka katika Shule ya Msingi Bugela, Ngilimba, Muge-ushetu, Mweli pamoja na Shule ya Msingi Shikizi ya Mkondogwa.

Wengi wa wanafunzi hao wanadaiwa kukatisha masomo kwa kubeba ujauzito, huku wengine wakipanga vyumba na kushindwa kujihudumia.

Mwalimu Mkuu wa Sekondari ya Ulowa, Godfrey Msimbe aliyabainisha hayo juzi wakati akitoa taarifa ya uanzishaji wa sekondari hiyo mbele ya Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani.

Cherehani alifika katika kijiji hicho kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi katika sekta ya elimu, afya, maji na kilimo.

Alisema, kutokana na wanafunzi kutembea umbali mrefu, serikali ya kijiji kwa kushirikiana na wazazi walilazimika kuchangisha fedha na kununua eneo lenye ukubwa wa hekari 12 kwa ajili ya uanzishaji wa sekondari mpya katika Kijiji cha Ingilimba kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wanatimiza ndoto zao.

Aidha, Msimba alisema wamepokea Sh. milioni 603 za uanzishaji wa sekondari hiyo na wanatarajia kujenga jengo moja la utawala, maabara tatu za masomo ya sayansi, maktaba, jengo la Tehama, matundu nane ya vyoo pamoja na vyumba nane vya madarasa ili kuanza masomo na kuondoa adha hiyo.

"Sekondari hii ya Ulowa ina zaidi ya wanafunzi 1,000 na wengi wanatoka katika vijiji hivi, kutokana na kutembea na umbali mrefu serikali ya kijiji kwa kushirikiana na wazazi wamenunua hekari 12 za kuanzisha ujenzi wa sekondari mpya,"alisema Msimbe.

Akizungumza kwa niaba ya wazazim Hamim Hashimu alisema, awali walinunua hekari nane baada ya kuona ni ndogo, mmoja wa wakazi alijitolea eneo lenye hekari 12 ili kufanikisha ujenzi wa sekondari, lengo ni kuhakikisha wanafunzi hasa wa kike wanatimiza ndoto zao na kuja kuwasaidia hapo baadaye.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema ujenzi wa sekondari hiyo unatarajia kuanza julai 21, na unatarajia kukamilika Oktoba 30, mwaka huu ili mwakani ianze kutoa huduma kwa wanafunzi hao.

Hata hivyo Cherehani aliwataka wananchi kushiriki katika shughuli ndogo ndogo zitazokuwa zinafanyika wakati wa ujenzi ikiwa ni pamoja na ubebaji wa mchanga na maji.

Pia, aliwasihi kuwa makini na vifaa vya ujenzi na wasijihusishe katika wizi ambao utasababisha ujenzi kutokamilika kwa wakati.

Alisema kwa wale watakaobainika wahakikishe wanawaripoti ili wachukuliwe hatua za haraka za kisheria.

ama

ALHAMISI JULAI 20, 2023

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## Kitisho cha joto kali kinapolipuka tena Ulaya na Asia sasa ni nyuzi 50



## Mchawi kudorora huduma za afya vituoni, zahanati, hospitalini huyu hapa

Ukurasa 12

# Rukwa sasa yaelekea kuandika historia kutokomeza mimba na ndoa za utotoni

**Na Zuwena Shame, RUKWA**

RUKWA ni miongoni mwa mikoa 10 bora vinara kwa idadi kubwa ya ndoa na mimba za utotoni ikifikia asilimia 40 ikimaanisha kuwa katika mabinti 100 arobaini ni wajawazito, kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Watoto Duniani (UNICEF).

Shinyanga ni wa kwanza ukiongoza kwa asilimia 59, Tabora 58, Mara 55, Dodoma 51, Lindi 48, mingine inayofuatia ni pamoja na Mbeya 45, Morogoro na Singida 42 wakati Rukwa ni asilimia 40.

Mkoa huo unakadiriwa kuwa na mabinti 77,412 wenye miaka kati ya 15 hadi 19 ambao asilimia 29 ya wasichana hao wameshapata mimba au wana watoto.

Licha ya mahakama kutaka Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 irekebishwe, inalalamikiwa kuwa inamruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri wa miaka 14 kwa ridhaa ya wazazi, walezi na miaka 15 kwa ridhaa ya mahakama, wakati wa kiume anaruhusiwa kuoa akiwa na miaka 18.

Ndiyo sababu watetezi wa haki za watoto wanasema ndoa hizo za utotoni ni ukiukwaji wa haki za msingi ikiwamo usawa, utu na kupata elimu.

Tanzania inaruhusu mwanafunzi kuendelea na masomo baada ya kujifungua, lakini wasichana bado wanakumbana na changamoto katika kumalizia elimu yao.

Jitihada mbalimbali za wadau likiwamo Shirika la Plan International kupitia mradi wa Tanzania Girl's Get Equal Integrated, zinadhamiria kuinua wasichana kupata haki ya msingi ya elimu kwa kupinga mimba na ndoa utotoni.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. **PICHA: MTANDAO**

Utafiti unaofanywa na Nipashe kwa kushirikiana na Plan International wilayani Kalambo, Nkasi na Sumbawanga Vijijini Mkoa wa Rukwa hivi karibuni, unaonyesha kuwa mimba na ndoa za utotoni zinapungua.

Utafiti huo unaowahoji maofisa elimu, viongozi wa dini, wahudumu wa afya, wahamasishaji rika na viongozi wa serikali, wasichana na kamati za vijiji mradi unapotekelezwa katika kata 10 kati ya 27, unatoa picha hiyo.

Takwimu mkoani hapo zilibainisha kuwa mwaka 2019 zilikuwa mimba 32 zilizoripotiwa ikielezwa kuwa kwa kiasi kikubwa zilichangiwa na ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi salama kati ya vijana rika.

Sababu nyingine zilizochangia mimba hizo miaka ya nyuma ni umbali mrefu kutoka na kwenda shuleni na kukosa chakula shuleni, aidha mazingira yasiyo salama kwa wanafunzi pia yanatajwa.

Mwaka 2020 Plan International Tanzania ilipotekeleza mradi wa Girls Get Equal Integrated, mkoani Rukwa kwa kushirikiana na wadau kama Youth Employment Through Skills Enhancement (YES), mimba zilipungua hadi 20.

Ni baada ya kuongezeka uelewa kwa walimu shuleni, kuanzisha klabu za masuala afya ya uzazi na vita dhidi ya ndoa za utotoni, kadhalika kuongeza wahamishaji rika kueneza uelewa zaidi kuanzia shuleni hadi nyumbani.

Ofisa Elimu Sekondari Sumbawanga, Fanikio Bitende, anasema kuanzia 2021 hadi 2022, mimba zilishuka hadi saba, baada ya kuongezeka kwa elimu ya uzazi salama, kupinga ndoa na mimba utotoni na huku jamii zikielewa umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike na kuwapeleka shuleni.

Aidha, anataja kuwa ni kuanzishwa huduma rafiki za afya ya uzazi na upatikanaji wa taulo za kike shuleni na kupungua utoro hivyo mwaka jana hadi Juni mwaka huu zikaripotiwa mimba mbili ikionyesha ni mafanikio makubwa zaidi.

Aidha, Fanikio Bitende, anataja jitihada za klabu shuleni, jamii na viongozi wa dini, wazazi, walezi na waelimisha rika kuendelea kusambaza na kueneza elimu ya afya ya uzazi salama.

Pia utafiti unabaini kuongezeka kwa ufaulu kwa madarasa ya mitihani ya taifa, kidato cha nne, kama Ofisa Elimu Sekondari anavyosema kuwa mwaka 2019-2020 ulipanda hadi asilimia 80.2, mwaka 2021 hadi mwaka jana ufaulu ulikuwa asilimia 90.

"Hii imechangiwa na kuongezeka kwa uelewa wa umuhimu wa elimu, mazingira salama shuleni na ushirikiano wa mashirika kama Plan International." Anasema Bitende.

Upande wa shule za msingi, Wilaya ya Sumbawanga pia idadi ya mimba kwa wasichana imepungua ambapo mwaka 2019 zilikuwa nane na kupungua hadi tatu kutoka mwaka 2020-2022 na mwaka huu ni mbili, anaongeza Ofisa Elimu Sekondari.

Anasema mafanikio hayo ni matokeo ya kutoa elimu ya uzazi salama, kupungua utoro na kuboresha vifaa na miundombinu mbalimbali, vilevile kuhusisha wazazi na walezi kupitia Ushirikiano wa Wazazi, Walezi na Walimu (UWAWA) na kamati za vijiji.

Ufaulu kwa darasa la saba na la nne umeongezeka pia kwa miaka ya sasa ijapokuwa kupungua kwa

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Mchawi kudorora huduma za afya vituoni, zahanati, hospitalini huyu hapa

•Ni kamati na bodi za usimamizi, hazijulikani kwa watu, haziwajibiki

**Na Christina Mwakangale**

NI kama kila kona ya Tanzania kilio cha wagonjwa ni kukosa dawa hospitalini lakini kuandikiwa wakazinunue kwenye maduka yaliyoko nje ya mageti ya hospitali au vituo vya afya.

Aidha, kuna malalamiko lukuki kama kukosa maji hata kwenye wodi za wazazi na wagonjwa kulazimika kuishi na ndoo za maji mawodini, wengine kupeleka jiko au kuni ili kuwapikia jamaa wanaowauguza na uhaba wa miundombinu kama tanuri la kuteketeza taka za hospitalini.

Hayo yanatokea licha ya kuwapo kamati za usimamizi kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali ili kufuatilia uwajibikaji na weledi zinazoundwa ili kufuatilia mwenendo wa utoaji wa huduma.

Zipo kamati na bodi ambazo zimepewa mamlaka na serikiali kuhoji, kutoa ushauri na kufuatilia mwenendo wa uwajibikaji katika maeneo ya kutolea huduma za afya.

Itakumbukwa kuwa baada ya kujenga miundombinu, kuweka vifaa tiba na watoa huduma, kinachofuata ni kuzipa kazi Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya na Bodi za Kusimamia Hospitali za Halmashauri, zilizowekwa kisheria, kutathmini hali ya uwajibikaji kwenye utoaji huduma za afya katika sehemu hizo.

Wajumbe wa kamati hizo hutoka maeneo yanayozunguka kituo cha afya au hospitali, kwa kuwa wao ndiyo wanaishi na jamii na kufahamu changamoto za huduma hiyo, ufumbuzi na panapohitaji kupewa kipaumbele.

Utafiti uliofanywa na Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), kwenye wilaya mbili za Mbarali mkoani Mbeya na Handeni Tanga, umebaini kuwapo kwa uelewa duni miongoni mwa jamii kuhusu kazi ya kamati na bodi na inavyoelekea wengi hawazifahamu.



Profesa Stephen Maluka Mratibu wa Mradi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Mtafiti kutoka chuo hicho, Profesa Stephen Maluka anasema kazi iliyofanyika Julai hadi Oktoba mwaka jana, ikishirikisha wananchi 1,184, inabaini kuwa takribani asilimia 96 ya wanaohojiwa wanasema hawajawahi kupata mrejesho kutoka kwa wajumbe wa kamati na bodi hizo.

Kadhalika, Profesa Maluka ambaye ni mratibu wa mradi huo, anasema asilimia 49.8 ya wajumbe hao hawawajibiki katika kuyakusanya maoni kuhusu huduma za afya kwenye jamii.

"Asilimia 85.3 walikuwa hawajui kama kuna Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya na asilimia 96.5 hawana habari za kuwepo Bodi ya Afya ya Halmashauri, anabainisha.

Anasema pia utafiti unabaini asilimia 88.3 ya wanaohojiwa hajawahi kusikia wala kushiriki kuwachagua wajumbe wa kamati za usimamizi na bodi ya afya ya halmashauri takribani asilimia 91.7 hawafahamu chochote kuhusu majukumu ya vyombo hivyo.

"Ni asilimia 44.7 ya watu inayosema Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya na Bodi ya Afya ya Halmashauri, zina umuhimu wakati 14.5 wanasema wajumbe wanawajibika kwa wananchi," anaongeza.

**LENGO LA UTAFITI**

Akieleza kuhusu mradi huo ambao umelenga kuimarisha utendají kazi wa kamati na bodi nchini, Dk. Cresencia Massawe, mhadhiri kutoka DUCE, anasema utafiti huo unalenga kutathmini uelewa wa wananchi na uwajibikaji wa kamati na bodi kwa umma.

"Kamati hizi na bodi, zimeundwa kisheria na zinapaswa kupata mwakilishi. Tanzania mwaka 2001 iliunda sera ya kuanzishwa kwa Kamati za Afya kwenye vituo vya afya, mwaka 2017 serikali iligatua madaraka kwa vituo vya afya vikipewa mamlaka ya kujitengenezea mipango yao kuanzia kuomba fedha moja kwa moja. "

Anasema tangu mwaka 2017 vituo vilifungua akaunti zao na kamati zinasimamia rasilimali watu na fedha, kwa mujibu wa Dk. Crezencia.

Anaongeza kuwa wajumbe wa kamati hizo na bodi, huwawakilisha wananchi na pia katibu ni mganga mkuu wa kituo cha afya au zahanati.

"Tulikuja na utafiti eneo hilo kwa sababu kwenye ugatuzi wa madaraka kamati zimeongezewa majukumu ya kuhakikisha wanasimamia fedha, fungu linalotoka serikalini ili zitumike kwa tija." Anasema.

Anasema pia kamati hizo zina majukumu ya kusimamia huduma ili ziwe bora, pia katika vituo kuna fedha zinazokusanywa za malipo ya papo kwa papo, bima za mfuko wa afya wa jamii (CHF) ili zitumike ipasavyo, kwa hiyo ukimuacha mtoa huduma mwenyewe, uwajibikaji unaweza usiwe wa kiwango kinachohitajika.

Umuhimu wa kamati kila kituo, anasema kunaongeza uwajibikaji hasa kwenye kutoa huduma bora, matumizi ya fedha kwa kuwa watia saini ni mwenyekiti wa kamati, iliyoundwa kwenye eneo analoishi.

"Kituo ili kuweze kununua dawa kuna mchakato ambao mtia saini lazima aidhinishe, ili kutoa fedha. Ukiangalia kamati zipo na wananchi waliohojiwa wanasema bodi na kamati ni muhimu, ila utendaji kazi ndio tatizo," anabainisha Dk. Crezencia.

Anasema kuna umuhimu wa kamati hizo ambazo zipo kuanzia ngazi ya kituo cha afya, zahanati hadi hospitali ya wilaya, mikoa na taifa ambako huko kuna na bodi ili kuleta ufanisi na uwajibikaji.

"Kabla ya kwenda maeneo ya utafiti tuliangalia mifumo ya utendajikazi kiafya kwenye wilaya, kabla ya kuchagua wilaya hizo mbili, tulichagua moja ambayo inafanya vizuri na nyingine haifanyi vizuri sana.Tukaangalia je, kuna majibu tofauti. Tulichokiona kamati za Handeni na Mbarali, inasanifu picha ya kamati za afya kwa Tanzania," anasifu Dk. Crezencia.

## RUKWA SASA YAELEKEA KUANDIKA HISTORIA KUTOKOMEZA MIMBA NA NDOA ZA UTOTONI

**Inatoka Uk. 11**

ufaulu mwaka jana kumechangiwa na mrundikano wa wanafunzi madarasani na ukosefu wa walimu wa kutosha, Ofisa Elimu anasema.

Anaongeza kuwa mafanikio ya kupungua kwa mimba na ndoa za utotoni zimechangiwa na ushirikiano mkubwa kati ya serikali na wadau akitaja Plan International, wazazi, walezi viongozi wa dini kwamba ni suala linalohitaji nguvu na jitihada zaidi.

Mtoa huduma rafiki kwa vijana kituo cha afya Nkomoro Wilaya ya Nkasi, Scola Sunga, anataja uwepo wa mwamko kwa vijana wengi kuhusu afya zao na kutumia njia za uzazi wa mpango na kuhimiza kuwekeza katika ustawi wa kumwezesha msichana kuwa na mafanikio zaidi.

Scola anasema ni vyema kuboresha sheria zinazokataza ndoa utotoni, kutoa elimu ya kujamiiana kwa ufasaha, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa vijana.

Mwenyekiti wa klabu ya wazazi kata ya Matai A, Isaac Sawala, anasema maendeleo na ustawi wa jamii yanategemeana na afya, elimu na kumwezesha msichana hivyo ni vyema jamii kushikamana kutokomeza mimba na ndoa za utotoni ili wawe na maisha yenye mwanga.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Ziwa Tanganyika mikoa ya Katavi na Rukwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maridhiano ya Amani kwa Viongozi wa Dini Rukwa, Ambele Mwaipopo, anasema imani inafundisha kulinda na kulea vijana na kuitaka jamii nzima kushirikiana kupinga na kuzuia mimba na ndoa za utotoni.

Mwaipopo anaongeza kuwa viongozi wa dini wana jukumu la kuongoza jamii katika haki na hivyo watetee ustawi na kumwezesha msichana kielimu.

Meneja wa mradi wa Girls Get Equal Integrated, Ending Child Early an Forced Marriage Rukwa, Kisasu Sikwalanga, anasema ndoa na mimba hizo zimeendelea kuwa changamoto mkoani Rukwa.

"Hata hivyo jitihada na mipango mbalimbali imeonyesha matokeo chanya katika kupunguza tatizo hilo."

Sikwalanga anasema jitihada endelevu zinahitajika kuongeza elimu, kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, kumwezesha msichana kufanya maamuzi sahihi na ushirikiano baina ya wadau katika ngazi za jamii, mkoa na taifa ni muhimu kutokomeza vyanzo vya kiini cha ndoa na mimba utotoni mkoani Rukwa.

Anataja baadhi ya mapendekezo ya utafiti kuwa ni kutetea ujio sheria ya ndoa inayoweka miaka 18 kuwa umri wa kuwa na ndoa kwa jinsia zote, kufanya kazi na taasisi za serikali katika kuendeleza na kutekeleza sera ambazo zinalinda haki za mtoto wa kike na kutoa adhabu kali kwa wanaojihuisha na ndoa za utotoni.

"Pia kufanyike kampeni kubwa ya kutoa elimu katika ngazi za jamii, kimkoa na hata kitaifa kuelimisha jamii kuhusu madhara ya ndoa na mimba za utotoni, vilevile kuwahusisha watu muhimu katika jamii, vijana, watu maarufu na vyombo vya habari kuhamisha ujumbe chanya na mabadiliko ya tabia," anasema Sikwalanga.

AFYA

# 'Kwa Mama Samia ukatili kijinsia hauna nafasi tena'

**Na Sabato Kasika**

JUHUDI za kupambana na vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia, zinazozorotesha afya za kinamama, watoto na mabinti zinalenga kuifanya Tanzania kuwa huru bila uonevu.

Mara kadhaa, kazi hiyo imekuwa ikikumbana na changamoto mbalimbali, ikiwamo uelewa mdogo kuhusu masuala ya sheria na haki za binadamu.

Matokeo yake, vitendo hivyo vimekuwa vikiendelea huku vikigusa zaidi wanawake na watoto, kuanzia vipigo, ubakaji, ulawiti na aina nyingine za ukatili huo ambazo zinaweza kuathiri afya za maadhura au waathirika.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeanzisha vituo viitwavyo mkono kwa mkono au one stop centre katika maeneo mbalimbali nchini ambavyo hupokea maadhura na manusura wa vitendo hivyo na kuwapa huduma ya kwanza ya kiafya, kisaikolojia na kisheria kabla ya hatua zaidi.

Vituo hivyo vina watu muhimu wote kuanzia daktari, ustawi wa jamii, wanasheria, polisi, wataalamu wa saikolojia, ili kila mmoja kusaidia kutoa huduma kabla ya hatua nyingine zaidi kuchukuliwa.

Hayo yabainishwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, katika ufunguzi wa warsha kwa vyombo vya habari kuhusu kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia, inayofanyika jijini Dar es Salaam.

Pamoja na juhudi hizo za kuanzisha vituo hivyo, anasema bado kuna matukio ya ukatili wa kijinsia na mengine ambayo yanaendelea kuwapo na kwamba sasa serikali imekuja na kampeni maalumu.

Anaitaja kampeni hiyo ya kitaifa kuwa ni Mama Samia 2023-2025 yenye lengo la kutoa elimu ya kutokomeza ukatili huo katika jamii, ili iweze kuwa salama bila migogoro.

"Tumekuja kampeni iitwayo Mama Samia 2023-2025 au 'Mama Samia Legal Aid Campaign' kwa nchi nzima, kuijengea watu uelewa ili kutokomeza ukatili wa kijinsia ndani ya jamii," anasema Dk. Ndumbaro.

Waziri huyo anasema ukatili wa kijinsia una uhusiano wa karibu na suala la afya, kwa maelezo kuwa kipigo, ulawiti, ubakaji vyote walio tendewa wanahitaji huduma afya ili waweze kupona.

Anafafanua kuwa tangu mwanzoni mwa mwaka huu walianza kampeni hiyo katika mikoa ya Manyara, Dodoma na Shinyanga na sasa ni zamu ya mkoa wa Ruvuma kisha watakwenda kwingine.

"Kila mkoa tunafanya kampeni kwa siku 10 katika halmashauri zote na vijiji 30. Sasa tunakwenda mkoani Ruvuma, tutakuwa huko kuanzia Julai 22 mwaka huu, tunataka haki inapatikana kwa wakati," anasema.

WALENGWA

Waziri anawataja walengwa ni wananchi wote wanyonge walio pembezoni, wanawake na watoto, watu wenye mahitaji maalumu, wazee, wagane na wajane, wafungwa na watoto walio vizuizini, watumishi wa nyumbani na watu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ambao wamekuwa wakitendewa ukatili wa kijinsia.

"Wengine ni viongozi na wajumbe wa mabaraza ya ardhi na serikali za vijiji, kata, shehia, vitongoji, wajumbe wa shina, wadau wa maendeleo, asasi za kiraia, viongozi wa dini, watu mashuhuri, viongozi wa kimila, vyombo vya habari na wanajamii ni miongoni mwa walengwa.

"Kwa ujumla ni kwamba utoaji wa elimu ni jambo la muhimu katika vita hii, ili kuijengea jamii uelewa na kuwa tayari kukemea vitendo viovu au kutoa taarifa za vitendo hivyo kwenye vyombo vya dola," anasema.

**MPANGO**

Waziri Dk. Ndumbaro anasema kampeni hiyo itatekelezwa kwa kuzingatia mpango wa kuwajengea uwezo waelimishaji jamii ambao watatumika kutoa elimu maeneo mbalimbali na kuweza kuifikia jamii kama watu mashuhuri, viongozi wa kimila, kimila na wa dini.

"Hili ni kundi linaloaminika na jamii, linaloweza kushirikiana na serikali katika kampeni hii na kuleta matokeo chanya, lakini mpango mwingine ni uhamasishaji na kipengele hicho kitahusisha mbinu mbalimbali zinazoikutanisha jamii kwa pamoja kufikisha ujumbe," anasema.

Ataja mpango mwingine katika hilo kuwa ni kufanya kampeni ya msaada wa kisheria vyuoni na shuleni, na kwamba wataandaa nyenzo za elimu kwa umma, ikiwamo vipeperushi, miongozo na stika, kuandaa mpango wa tathmini na ufuatiliaji, kwa lengo kupima matokeo ya kampeni hiyo.



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumaro, alipofungua warsha ya waandishi wa habari kuhusu ukatili wa kijinsia.

**KUHAMASISHA**

Anafafanua kuwa kampeni hiyo ya kitaifa ya msaada wa kisheria ya Mama Samia 2023-2025, itahusisha wizara, wakala, taasisi na idara za serikali, mahakama za Tanzania, TAMISEMI, wadau wa maendeleo, asasi za kiraia, wanazuoni, vyombo vya habari, vikundi vya kijamii na sekta binafsi.

Mchumi Mkuu wa wizara hiyo, Ernest Mbuna, anasema utoaji wa elimu kupitia vyombo vya habari pamoja na uhamasishaji kupitia wadau mbalimbali ni nguzo muhimu ya kufanikisha kampeni hiyo.

"Kwa hiyo tunawaomba tushirikiane katika kampeni hii inayokwenda kwa muda miaka mitatu, kalamu zenu ni msaada mkubwa katika kuelimisha umma kuepuka unyanyasaji na ukatili wa kijinsia," anasema Mbuna.

Anasema katika mikoa ambayo kampeni hiyo imefika, walikuta vitendo hivyo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia huku migogoro ya ardhi ikiwa juu, hasa kwa wanawake kuzuiwa kumiliki ardhi.

"Mchango wenu kama waandishi wa habari utasaidia katika kampeni hii ya kitaifa, hivyo tuendelee kushirikiana, kwani tunakwenda kila halmashauri na kutoa elimu katika vijiji 30 kwa muda wa siku 10. Kampeni hii hadi ikamilike mwaka 2025, inatarajia kugharimu Sh.bilioni 52.651," anasema.

Anataja vyanzo vya fedha hizo ni kutoka serikalini, wadau wa maendeleo, wahisani, michango kutoka mashirika yanayotoa msaada wa kisheria, taasisi binafsi na wafanya biashara.

Wakili wa wizara hiyo, George Molell anasema jamii bado ina uelewa mdogo kuhusu sheria mbalimbali za nchi, kampeni inakwenda kwa kufanya watu kuwa na uelewa wa haki zao.

Anatoa mfano tukio la mkoani Shinyanga kwamba kupitia kampeni hiyo, waliweza kuvunja ndoa ya mwanafunzi na kumrudisha shuleni kuendelee na masomo.

Wizara inawajibika kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati, na kupitia kampeni hii itanufaika kwa kujiongezea uelewa wa kuhusu haki na wajibu na kupambana na ukatili wa kijinsia," anasema Molell.



Waandishi wakiwa kwenye warsha hiyo. **PICHA: ZOTE: SABATO KASIKA**

MAZINGIRA

# Kitisho cha joto kali kinapolipuka tena Ulaya na Asia sasa ni nyuzi 50

## •Ni kali halivumiliki kama nusu kiwango kufikia kuchemka maji



Hati hati za kunywa na kujimwagia maji kupoza mwili nchini Italia. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

ULAYA na mataifa mengine duniani mwaka huu yanaendelea tena kukabiliwa na wimbi la joto kali, hali inayochangiwa na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa, inaripoti DW.

Mabadiliko hayo yanaongeza joto, upepo, mafuriko, vimbunga na hata baridi, sasa viongozi wa mataifa hayo wanaonya juu ya hatari za kiafya na kuwataka watu kuchukua tahadhari kwa kunywa maji kwa wingi na kujikinga na jua kali.

Viwango vya joto vimevunja rekodi Jumanne wiki hii barani Ulaya na maeneo mengine duniani mfano ni kutoka jimbo la California huko Marekani hadi nchini China, kwa mujibu wa DW.

Wimbi hilo la joto kali halionyeshi dalili zozote za kupungua, hali hiyo ikishuhudiwa barani Ulaya kwenye visiwa vya Italia vya Sardinia na Sicilia ambako litafikia zaidi ya nyuzi joto 48.8 katika kipimo cha Celsius.

Ugiriki inakabiliwa na mioto ya misitu iliyowalazimu watu kuyakimbia makazi yao. Kaskazini-magharibi mwa mji mkuu Athens, wingu kubwa la moshi lilitanda kwenye msitu wa Dervenohoria na katika mji wa bahari wa Kouvaras, huku huduma za dharura zikipambana na mioto ya misitu katika maeneo mbalimbali karibu na mji mkuu na kwa siku ya pili.

Mji maarufu wa pwani wa Loutraki unakabiliwa pia na mioto ya misitu, ambapo Meya wa mji huo amesema watoto 1,200 wamehamishwa kutoka sehemu za mapumziko ili kuepusha hatari.

Huko Italia, mamlaka za afya zimetangaza kuanzia wiki hii kwamba hali ya tahadhari kwa miji 20, kutoka kusini mwa Napoli hadi kaskazini mwa Venice ambapo viwango vya joto vinatarajiwa kufikia nyuzi joto 44 C huko Catalonia na katika visiwa vya Balearic.

Aidha, DW inasema mji wa Lanusei karibu na pwani ya mashariki ya Sardinia, hatua kadhaa zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na watoto kuruhusiwa ucheza ufukweni nyakati za asubuhi wakati jua halijawa kali na si vinginevyo.

Kwenye jiji la Roma ambako kunatarajiwa hadi nyuzi joto 42 katika kipimo cha Celsius, watu wamebadili mfumo wa mavazi na hata chakula, wakipendelea kuvaa nguo nyepesi na kula vyakula laini kama 'kachumbari' au mboga.

> “Ofisa wa afya katika eneo la Ballia S.K Yadav anasema karibu watu 300 walilazwa katika hospitali ya wilaya kwa maradhi yaliyochochewa na joto kali.

Aidha, baadhi ya wakazi huko Cagliari wameripotiwa kupatwa na presha ya kushuka kutokana na joto kali na kutishia hali za afya.

### WMO NA ANGALIZO

Wito wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Hali ya Hewa Duniani (WMO) ni kuwakumbushia binadamu kuhusu athari za ongezeko la joto duniani na kusema dunia inapaswa kujiandaa kwa mawimbi yanayoongezeka ya joto kali.

John Nairn, mshauri mkuu katika shirika hilo la WMO anasema: “Tunashuhudia ongezeko la matukio haya mara kwa mara na viwango vya juu vya joto. Na hii inaendana na tafiti zote kuhusu ongezeko la joto duniani. Matukio haya yataendelea kuongezeka kwa kasi na dunia inapaswa kujiandaa kikamilifu kukabiliana na mawimbi ya joto kali.”

Mwezi uliopita karibu watu 100 walikufa nchini India kutokana na joto kali lililolikumba taifa hilo, inasema DW.

Walikufa katika majimbo mawili yenye idadi kubwa zaidi ya watu ya Uttah Pradesh lililoko magharibi mwa nchini hiyo na Bihar, lililopo upande wa mashariki, huku maofisa wakiwataka wakazi na hasa wa miaka 60 na zaidi na wenye maradhi mbalimbali kukaa ndani nyakati za mchana.

Habari zilisema kuwa waliokufa ni wazee wa zaidi ya miaka 60 na wenye matatizo ya kiafya, na huenda joto kali lilichochea vifo vyao kuliko makundi mengi ya watu hasa vijana.

Ofisa wa afya katika eneo la Ballia S.K Yadav anasema karibu watu 300 walilazwa katika hospitali ya wilaya kwa maradhi yaliyochochewa na joto kali.

### KWANINI JOTO HUUA?

Ni swali ambalo pengine watu wanajiuliza. Wakati mwingine joto husababisha kushindwa kupumua.

Lakini kubwa zaidi linachangia upungufu mkubwa wa maji mwilini, unaotokana na kutokwa jasho jingi muda wote.

Aidha, pia huleta hali inayoitwa 'cerebrovascular' ugonjwa unaoziathiri njia na mishipa ya damu ya ubongoni na mzunguko mzima wa kazi za ubongo.

Kwa ateri au mishipa inayosambaza oksijeni na virutubisho kwenye ubongo mara nyingi huharibiwa au kuharibika katika tatizo hilo.

Kwa upande mwingine, joto ni chanzo cha 'thrombogenesis' au kuganda kwa damu mwilini hivyo ubongo, mapafu na tishu zote kukosa chakula na hewa safi kazi inayofanywa na damu isiyoganda na matokeo yake ni kifo.

Watu wenye magonjwa ya muda mrefu wanaotumia dawa za kila siku wana hatari kubwa ya matatizo na kifo wakati wa joto la joto na waathirika wakubwa ni pamoja na wazee na watoto.

Kukiwa na joto kali mwili wako hujipoza kwa kutokwa na jasho jingi ukitoka jasho mwili hupoa, lakini joto linapozidi maji yatatoka kupita kiasi na huenda yakamilizika mwilini na kukakosekana unyevunyevu kwenye ngozi, tishu za mwili na matokeo yake ni kukakamaa na kupata shida ya kubanwa misuli ya tumbo, moyo, ini na viungo vingine hali inayosababisha kifo mara moja.

Wataalamu wa afya wanashauri kunywa maji kwa wingi, kuepuka kukaa juani wakati wa wimbi la joto ili kuwa salama zaidi, si vyema pia kwenda ufukweni au kuingia baharini na hata wakati mwingine inashauriwa kupunguza au kuachana na mazoezi ya viungo yanayosababisha mwili kutoka zaidi jasho. Ni kwa mujibu wa mtandao wa MAYO.



# Mkakati kushughulikia migogoro ya ardhi kuzinduliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya Jiji la Dodoma kutajwa kuwa kinara wa migogoro ya ardhi nchini, uongozi wa mkoa huo umezindua mkakati maalum wa kushughulikia tatizo hilo kwa mwaka mmoja na utahusisha wataalamu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Akizindua mkakati huo jana, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema tangu kutangazwa rasmi kwa mpango wa serikali kuhamishia shughuli zake Dodoma Julai 25, 2016, Jiji hilo limeendelea kukua kwa kasi na kuvutia fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye sekta zote muhimu.

Alisema sekta hizo ni pamoja na huduma za kijamii, kiuchumi, biashara, ujenzi na uwekezaji wa miundombinu msingi.

"Kwa mujibu wa makisio ya mwaka 2022 ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Jiji la Dodoma linakadiriwa kuwa na wakazi takribani 765,179 ambao ni sawa na ongezeko la asilimia 16.2 la idadi ya wakazi wote waliokuwapo mwaka 2016," alisema.

Aidha, Senyamule alisema ongezeko hilo limesababisha uwepo wa mahitaji makubwa ya ardhi hususani la viwanja kwa ajili ya kukidhi matumizi ya shughuli za ofisi mbalimbali za umma na binafsi sambamba na biashara mpya zinazofunguliwa.

"Kimsingi Halmashauri ya Jiji la Dodoma kama ilivyo kwa halmashauri nyingine hapa nchini kwa sasa ni moja ya halmashauri zinazokabiliwa na kero za migogoro mingi ya ardhi," alisisitiza.

Alisema kwa kuzingatia hilo kumekuwa na jitihada mbalimbali ambazo zimekuwa zikichukuliwa na halmashauri ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Kamishna wa Ardhi Mkoa pamoja na Wizara ya Ardhi na vyombo vingine vya utatuzi wa migogoro katika kuipatia ufumbuzi.

Kadhalika, alisema kwa muda mrefu mamlaka mbalimbali za serikali zimekuwa zikijitahidi kutatua migogoro hiyo lakini imekuwa haiishi na wananchi kuendelea kulalamikia.

Alisema kwa uchunguzi uliofanywa na mkoa walibaini malalamiko mengi ni ya fidia na watu walioahidiwa kupewa viwanja mbadala.

"Kimsingi maelekezo mbalimbali yalikuwa yanatolewa ili kutafuta ufumbuzi wa suala hili lakini suluhu ilikuwa haipatikani kwa kuwa halmashauri ilikuwa haitoi kipaumbele katika kutenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia ikiwa ni pamoja na kupima viwanja kwa ajili ya kutoa kama mbadala wa kumaliza kero hizi," alisema.

Vile vile, alisema sauti za kero hizo zimeendelea kuwa kubwa na kuwafikia viongozi mbalimbali akiwamo Waziri Mkuu, Katibu Mkuu wa CCM, Mwenyekiti wa CCM Mkoa na viongozi wengine ambao pia wametaka kero hizi kupatiwa utatuzi.

Pia, alisema kwa kutambua kero hizo aliitisha kikao cha wadau wote wanaohusika katika kutatua tatizo hilo wakiwapo wataalamu wote wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma wakiongozwa na Mkurugenzi wa Jiji, Kamishana wa Ardhi Mkoa wa Dodoma.

Alisema kwa kushirikiana na wataalamu wa mkoa walijadili namna bora ya kumaliza tatizo hilo ambapo walikubaliana kuunda timu itakayoandaa mkakati maalumu wa kumaliza shida hiyo katika Jiji la Dodoma.

Alisema: "Napenda kuujulisha umma huu kuwa mnamo Julai 7, 2023 kamati hiyo imewasilisha mkakati huo ambao pamoja na hatua nyingine kama mkoa tumejipanga kuutekeleza ili kutatua migogoro ya ardhi Dodoma".

## BBT yaanza kuleta matunda, Bashe awapongeza vijana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewapongeza vijana wa programu ya BBT kwa kuanza kuvuna na kuuza mazao yaliyozalishwa kwenye kituo atamizi cha Bihawana kilichopo jijini Dodoma.

Akizungumza na baadhi ya vijana hao waliomtembelea ofisini kwake jana, Bashe aliwataka vijana hao kuweka jitihada kwa vitendo wa yale wanayofundishwa ili kujiinua kiuchumi baada ya kuhitimu mafunzo wanayopewa katika vituo atamizi vilivyotengwa na serikali.

"Nawapongeza sana kutokana na hiki mlichofanya, mmeonyesha jinsi gani mnazingatia kile mnachofundishwa kwa vitendo, endeleeni kuweka jitihada ili mtanue soko la mazao haya," alisema.

Bashe alisema kitendo walichofanya vijana hao kimeonyesha utayari wa kile ambacho serikali imeandaa kuwafanyia vijana kupitia sekta ya kilimo kupitia programu ya BBT.

"Nimefurahi sana kuona matokeo chanya kutoka kwenu vijana, endeleeni kufanya kazi kwa bidii ili mzidi kuonyesha matokeo yenye tija kwa taifa na kwenu vijana," alisema Bashe.

Aliwataka kutafuta masoko pia katika ofisi za umma ili kujua uhitaji wa mazao ya bustani kwa jamii.

Naye, mmoja wa wanufaika wa programu ya BBT, Asia Msuya, aliishukuru serikali kwa kuhamasisha vijana kushiriki katika kilimo biashara ambacho kinachangia kwa kiasi kikubwa kuinua jamii kiuchumi.

Msuya alieleza kuwa kupitia programu ya BBT, amepata maarifa ya kilimo na sasa yupo tayari kufanya shughuli za kilimo kwa weledi na kujipatia kipato ambacho kitamsaidia kujiinua kiuchumi yeye na familia yake.



Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi (kulia), akiwa katika ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Mashujaa katika eneo la Mtumba jijini Dodoma jana, inayotarajiwa kufanyika Julai 25, mwaka huu. Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## RC aagiza ujenzi shule za msingi kukamilika haraka

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewaagiza viongozi wa halmashauri za mkoani humo kuhakikisha miradi ya ujenzi wa shule mpya za msingi zinazojengwa kwa fedha za mradi wa Boost inakamilika wiki hii.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea na kuzikagua shule mpya za msingi zinazojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Mkalama, Singida na Manispaa ya Singida ambapo ujenzi wa majengo kwenye halmashauri hizo baadhi zimefikia 100 na nyingine kati ya asilimia 90 hadi 95.

Serukamba alisema katika miradi aliyoitembelea ameibaini mafundi wamewekwa wachache katika hatua ya umaliziaji wa kazi zilizobaki na hivyo kuagiza kuongeza mafundi ili kazi ya kumalizia majengo hayo ikamilike na Jumamosi akabidhiwe funguo za majengo.

"Ikifika Jumamosi wiki hii miradi yote ya Boost iwe imekamilika na sitatoa tena muda mwingine," alisema.

Aidha, amewaagiza wenyeviti wa vijiji na madiwani kuwahamasisha wananchi wao kufanya usafi katika shule hizo mpya zilizojengwa ili wanafunzi watakapoanza masomo yawe katika mazingira mazuri.

Alisema katika shule hizo mpya zilizojengwa walimu wahakikishe miti inapandwa na ili kufanikisha zoezi hilo wanafunzi wapewe miti ya kupanda na kuisimamia jambo ambalo litazifanya shule hizo kupendeza na kuwa na madhari mazuri.

"Tunapanga wiki ijayo tutakutana pale Minga kwa ajili ya kufanya sherehe kubwa ya kupokea mradi huu ambao mkoa wetu umepokea zaidi ya Sh. bilioni tisa na tuishukuru sana serikali," alisema.

Alisema serikali imejipambanua kwa kufanya kazi kubwa ya kuendeleza maisha ya watu kuwekeza kwenye maisha ya watu na vitu vinavyohusu watu.

"Kuwekeza kwenye elimu ni kuwekeza kwenye mtu mmoja mmoja, ukiwekeza kwenye afya umewekeza kwenye afya ya mtu mmoja kimsingi Rais Samia amefanya kazi kubwa sana sana, pia hajaacha sekta za uchumi kama umeme, barabara kuna kazi kubwa sana imefanyika," alisema Serukamba.

Aliongeza kuwa katika sekta ya umeme Mkoa wa Singida una vijiji 441 itakapofika Juni 2024 kila kijiji kitakuwa kimepata huduma ya umeme na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri alizofanya kwa Mkoa wa Singida.



# MV Mbeya II yafufuliwa, kuanza kazi muda wowote

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MELI ya MV Mbeya II ambayo ilikuwa imesimama kufanya kazi kwa zaidi ya mwaka mmoja kutokana na hitilafu kwenye mfumo wa injini, inatarajiwa kuanza kazi muda wowote baada ya ukarabati kukamilika.

Ukarabati wa injini hiyo umegharamiwa na Shirika la Bima la Taifa (NIC) ambalo limetumia zaidi ya Sh. milioni 309 mpaka kukamilika kwake.

Meli hiyo ilipata hitilafu Mei 2021 baada ya kupigwa na dhoruba katika ufukwe wa Matema ikiwa na zaidi ya abiria 80 hali iliyoilazimu serikali kuzuia isiendelee kubeba abiria mpaka ikarabatiwe.

Juzi, maofisa wa NIC walikabidhi meli hiyo kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA) kwa ajili ya kuendelea kuitumia baada ya ukarabati kukamilika.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo mwakilishi wa NIC, Hardbert Polepole ambaye ni Mkurugenzi wa Bima za Maisha, alisema ukarabati wa meli hiyo umekamilika na ipo tayari kwa matumizi.

Alisema Mkurugenzi Mkuu wa NIC, Dk. Elirehema Doriye, aliagiza ukarabati huo ufanyike kwa umakini ili kuhakikisha chombo hicho cha umma kinarejea na kuanza kufanya kazi.

Alisema shirika hilo linaendelea kuwa miongoni mwa mashirika bora kwenye kulipa fidia katika majanga hususani ajali na majanga mengine ambayo yanasababisha uharibifu wa mali na kugharimu maisha ya watu.

"TPA ni wadau wetu na hiki kilichotokea kwenye meli hii ilikuwa ajali hivyo sisi NIC Insurance tumeweza kusimamia ukarabati huu na leo (juzi) tunakabidhi rasmi kwa TPA baada ya kuwa sasa iko vizuri na inaweza kufanya kazi," alisema Polepole na kuongeza.

"Tumejiridhisha ukarabati huu uliokuwa chini ya kampuni ya ManTrack, meli iko tayari kwa shughuli zake hivyo wananchi wanaweza kuanza kuitumia kama kawaida kwa kusafiria na kusafirisha mizigo," aliongeza.

Kwa upande wake Mhandisi wa Meli kutoka TPA, Julius Mpinga, alisema ukarabati katika injini hatua ya kwanza ilianza Februari 2 hadi Juni 6 mwaka jana na kwamba hitilafu kubwa ilibainika eneo la piston.

Alisema baada ya marekebisho hayo waliamua kuijaribu kwa miezi nane na kubaini tatizo kumalizika na kwamba kwa sasa meli hiyo inaweza kufanya kazi kama ilivyokuwa awali kabla haijapata hitilafu.

Aliwatoa hofu wananchi wanaotumia usafiri huo kutoogopa kuitumia kwa maelezo kuwa kwa sasa iko vizuri na itaanza kusafirisha abiria.

"Meli hii ilifanyiwa marekebisho mwaka jana, baada ya hapo tuliijaribu majini kwa miezi nane na kujiridhisha iko sawa kwa kazi, hivyo tunaipokea rasmi na kuwaomba wananchi na wafanyabiashara kuendelea kuitumia," alisema Mpinga.

Alisisitiza kuwa meli hiyo pamoja na zingine mbili za mizigo zilijengwa na serikali kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa mwambao mwa Ziwa Nyasa kusafiri na kusafirisha mizigo yao.

Baadhi ya wananchi wa Mji wa Kyela waliishukuru serikali kwa kuikarabati meli hiyo wakidai kuwa ilipokuwa imesimama baadhi ya shughuli zao pia zilikwama.

Mmoja wa wananchi hao, Eva Mwakanyamale ambaye ni mjasiriamali anayeuza samaki katika Bandari ya Itungi alisema baada ya meli kuacha kufanya kazi wateja wa samaki walipungua kwa kiasi kikubwa.



Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, wakikagua mpaka mpya wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani Mbarali juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Dk. Stephene Mwakajumilo na (katikati) ni MNEC, Ndele Mwaselela pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwile. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Tume ya Bonde la Mto Songwe yapata bosi mpya

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BARAZA la Mawaziri la Bonde la Mto Songwe limemteua Dk. Ladislaus Kyaruzi, kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe.

Tume ya Bonde la Mto Songwe inaundwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Malawi ambapo mwaka 2019 Tanzania na Malawi zilizindua tume ya pamoja kwenye Bonde la Mto Songwe kwa lengo la kuendesha miradi ya umwagiliaji na uzalishaji wa umeme yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 829.

Dk. Kyaruzi ana Shahada ya Uzamivu katika mabadiliko ya tabia nchi na maendeleo endelevu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ameanza majukumu yake Julai 1, 2023, baada ya kuchukua nafasi ya Hyde Sibande.

Kabla ya uteuzi huo, Dk. Kyaruzi alikuwa Mkuu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) anayehusika na mazingira na maliasili.

Mwaka 2011-2021, alikuwa amehudumu kama mpatanishi wa kikundi cha kiafrika kinachojadiliana kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa kwa mchakato wa UNFCCC.

Dk. Kyaruzi pia ni mjumbe wa kamati tendaji ya teknolojia ya ulimwenguni kwenye mkataba wa mfumo wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabianchi (2018 hadi sasa).

Dk. Kyaruzi pia amewahi kusaidia kuratibu marekebisho ya Itifaki ya Jumuiya ya Usimamizi wa Mazingira na Maliasili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pia, aliratibu uendelezaji wa mkakati wa kitaifa wa mabadiliko ya tabianchi wa Tanzania.

Kwa upande wa uongozi na uhusiano na mashirika au taasisi zinazofanana za kikanda na kimataifa, kuanzia 2016-2017, Dk. Kyaruzi alikuwa Mwenyekiti wa Tawi la Uwezeshaji Duniani la Kamati ya Ufuatiliaji ya Itifaki ya Kyoto kwa mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabianchi.

Pia, aliwahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Tawi la Uwezeshaji Duniani la Kamati ya Ufuatiliaji ya Itifaki ya Kyoto tangu mwaka 2014 hadi 2015.

Vilevile kwa mwaka 2013-2014 alikuwa mjumbe wa timu ya wataalamu kutoka Tanzania kwa Mratibu wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika kuhusu mabadiliko ya tabia nchi.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alimpongeza Dk. Kyaruzi kwa kuteuliwa na kusema ana imani kuwa, Tume ya Bonge la Mto Songwe iko katika mikono salama.

## CCM yakagua mpaka Hifadhi ya Ruaha, wananchi Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, imeanza kukagua mpaka mpya kati ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wananchi wilayani Mbarali kwa lengo la kupata maoni ya wananchi.

Mpaka huo umetengenezwa baada ya serikali kuamua kurekebisha ule wa awali uliokuwa umetangazwa kupitia Tangazo la Serikali Namba 28 (GN. 28) la mwaka 2008 ambao ulikuwa unasababisha migogoro kutokana na kuchukua maeneo makubwa ya wananchi.

Katika kukabiliana na tatizo hilo Serikali ya Mkoa wa Mbeya iliunda timu ya wataalamu wa kupita upya mpaka huo na kuandaa mapendekezo ya namna ya kutatua mgogoro uliokuwapo baina ya wananchi na hifadhi.

Timu hiyo iliandaa mapendekezo ambayo baadaye yaliridhiwa na timu ya mawaziri wanane wa kisekta ambao pia walikuwa wanashughulikia mgogoro huo.

Hata hivyo serikali iliridhia mpaka huo kurekebishwa kwa kufuata mapendekezo ya timu ya mkoa pamoja na mawaziri ambapo zaidi ya hekta 74,000 zilirejeshwa kwa wananchi kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao.

Juzi kamati hiyo ilifanya ziara katika maeneo mbalimbali ikiwamo Kata ya Imalilosongwe ambayo ni miongoni mwa maeneo ambayo yameathirika zaidi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephene Mwakajumilo, alisema lengo la ziara hiyo ilikuwa kusikiliza maoni ya wananchi ili wapate kitu cha kuishauri serikali.

Alisema maeneo mengi wananchi wamepata nafuu kutokana na marekebisho hayo na kwamba kwa yale maeneo machache yaliyobakia na migogoro wataendelea kuishauri serikali.

"Tunaipongeza serikali kwa hatua hii iliyofikia, lakini kwenye maeneo machache ambayo yana shida bado tutaendelea kuyashughulikia," alisema Dk. Mwakajumilo.

Kamati hiyo ya siasa inaendelea na ziara katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya yenye lengo la kukagua miradi ya maendeleo, kusikiliza kero za wananchi na kukagua uhai wa chama.



## Jeshi la Polisi lataja dawa ya kutibu msongo wa mawazo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMANDA wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Rearch Mchomvu, ameitaka jamii inapokua na matatizo ni vyema kusimuliana ili kuepukana na madhara yatokanayo na msongo wa mawazo.

Alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kufuatia kijana mmoja kujinyonga kutokana na msongo wa mawazo.

Alisema mnamo Julai 17, mwaka huu huko Bububu kijana Abdulfath Hemed Bakari (25) alifariki dunia baada ya kujinyonga kwa kujitia kitanzi kwa kutumia mkanda wa habaya aina ya tetron.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni msongo wa mawazo, kwamba mbinu aliyoitumia ni kufunga kitanzi katika nondo ya dirisha chumbani kwake.

Alisema tukio hilo limetokea majira ya saa mbili usiku na mwili wa marehemu ulihifadhiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kukabidhiwa kwa ndugu zake kwa taratibu za mazishi.

Aidha, Kamanda huyo alisema ni vyema jamii inapokua na matatizo ni vyema kusimuliana ili kupata ushauri kuliko kujichukulia sheria mikononi.

Alisema: "Kujiua sio suluhisho ni vyema unapokua na jambo linalokukwaza kumtaarifu mwingine ili kukupa ushauri mzuri na unaostahiri."

**Alisema mnamo Julai 17, mwaka huu huko Bububu kijana Abdulfath Hemed Bakari (25) alifariki dunia baada ya kujinyonga kwa kujitia kitanzi kwa kutumia mkanda wa habaya aina ya tetron.**

# Dk. Mwinyi mgeni rasmi Wiki ya Msaada wa Kisheria

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria Zanzibar itakayofanyika, Julai 22 mwaka huu.

Maadhimisho hayo yatafanyika sambamba na utoaji tuzo kwa wasaidizi wa kisheria visiwani humo.

Akizindua maadhimisho hayo jana visiwani humo, Waziri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman alisema maadhimisho hao yanafanyika kwa ushirikiano na Taasisi ya Legal Services Facility (LSF).

Alisema wiki hiyo itakuwa mahusus i kwa ajili ya kutoa elimu pamoja na huduma za msaada wa kisheria katika jamii ili kuwafikia wananchi wengi zaidi wenye uhitaji wa huduma hiyo, na ni hatua ya serikali kuwajali wananchi wake.

Alisema maadhimisho ya wiki ya msaada wa kisheria Zanzibar yanafanyika huku yakipambwa na shughuli mbalimbali za kijamii lengo likiwa ni kuhamasisha jamii kufikiwa na huduma za msaada wa kisheria popote zilipo bila kikwazo.

"Miongoni mwa shughuli zitakazofanyika katika wiki hii ni pamoja na utoaji wa elimu ya kisheria kupitia vyombo vya habari, uendeshaji wa jukwaa la kona ya msaada wa kisheria ili kuyafikia makundi yote katika jamii.

Aliongeza kwa kusema: "Kutembelea makundi yaliyoko vizuizini (magerezani/rumande au vyuo vya mfunzo) pamoja uandaaji wa bonanza la msaada wa kisheria kwa ajili ya kupaza sauti kuhusu kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji katika jamii".

Aidha, alisema shughuli hiyo ni muhimu ili kuwa jamii yenye ustawi mzuri ulioimarika katika kila nyanja ya maisha pamoja na kuhakikisha wananchi wake hususani wanyonge na wasiojiweza wanapatiwa msaada wa kisheria bila ya usumbufu wowote.

Ofisa Programu Mwandamizi kutoka Legal Services Facility Zanzibar, Alphonce Gura, alisema kuwa wao ni wadau wakuu katika maadhimisho ya wiki ya msaada wa kisheria Zanzibar kwa kuwa tukio hilo linalenga kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi ili kuongeza upatikanaji wa haki pasina kikwazo chochote kile.

Alisema: "LSF kazi yetu kubwa ni kukuza upatikanaji wa haki kupitia uwezeshaji wa kisheria kwa wananchi wote hususani wanawake na wasichana. Hivyo kupitia maadhimisho haya tutaweza kuwafikia watu wote kupitia shughuli mbalimbali ambazo zinakwenda kufanyika katika kipindi hiki cha maadhimisho".



Baadhi ya vijana wafanyabiashara wakiwa katika ufukwe wa Bahari ya Hindi eneo la Kikwungwi, mkoa wa Kusini Unguja jana, wakijiandaa kusafirisha bidhaa kuelekea kisiwa cha Kwale kwa ajili ya kuwahudumia watalii wanaofika kisiwani humo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Askari aliyetuhumiwa kuingiliwa kimwili aachiwa huru

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MSHTAKIWA Ramadhan Hassan Ali aliyekuwa askari wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Kutuliza Ghasia ambaye alikabiliwa na kesi ya jinai ya kuingiliwa kimwili ameachiwa huru katika Mhakama ya Mkoa Vuga visiwani Zanzibar.

Mahakama hiyo imemuachilia huru mshtakiwa huyo baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kosa.

Akitoa hukumu ya shauri hilo namba 59 la 2023, Hakimu wa mahakama hiyo, Khamis Ali Simai alisema mshtakiwa hana hatia, hivyo amemwachia huru kwa mujibu wa Kifungu cha 220 cha Sheria Namba 7 ya Mwaka 2018.

Alisema katika mashahidi waliowasilisha hakuna shahidi aliyeeleza kuwa alimuona mshtakiwa akiwa anafanya kitendo cha kuruhusu kuingiliwa kimwili.

Aidha, alisema ushahidi wa upande wa mashtaka uliokua ukiongozwa na wakili wa serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), Mohmed Saleh ulikua na kasoro kubwa zilizoshindwa kuthibitisha kosa.

Alieleza kuwa jumla ya mashahidi tisa waliwasilisha ushahidi mahakamani ukiwamo ushahidi wa kielektroniki uliochukuliwa baada ya picha kusambaa mitandaoni wakati sheria za Zanzibar zinaeleza ili ushahidi huo ukubalike lazima ufuate masharti yaliyoelezwa katika Sheria ya Ushahidi ya Mwaka 2016 kifungu Namba 73(4).

Alisema kuwa mashahidi wote waliofika mahakamani pamoja na picha za video iliyosambaa mitandaoni hazikukidhi masharti ya kifungu hicho na taratibu zilizowekwa za kuwasilisha ushahidi.

Baada ya kumalizika kwa kesi hiyo wakili wa utetezi wa mshtakiwa, Hassan Kijogoo, aliiomba jamii kuacha kutoa hukumu juu ya mashauri yanayowakabili watuhumiwa wanaofikishwa mahakamani badala yake waviache vyombo hivyo kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Kesi hiyo ya jinai iliyokua ikimuhusisha mshitakiwa huyo ambaye ni askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia, ilifunguliwa Machi 20, mwaka huu baada ya picha zilizokua zikimwonesha mwanaume aliyedaiwa kuwa mshtakiwa huyo akiingiliwa kimwili kusambaa mitandaoni na kuanza kusikilizwa ushahidi Aprili 3, mwaka huu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



ESTHER MATHEW NG'ONG'A anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: S0938-0145 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MBEZI BEACH SECONDARY SCHOOL mwaka 2000. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: DAR/CHA/RB/152579/2023

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI......**
**148.....LA.. 2023**
**EPAFRA OSHORAEL**
**ANGA.....MUOMBAJI/WOMBAJI**
**DHIDI YA**
**LISUNGU**
**KIPIGAPASI............MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**LUSUNGU KIPIGAPASI**
**POPOTE ULIPO:**
EPAFRA OSHORAEL ANGA amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 25/7/2023 saa 3:00 asubuhi/mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 19 mwezi 07, 2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BWANA HANNINGTON STEPHEN** CHAWALA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T876 BHK,** MITSUBISHI CANTER ENGINE NO: **FE568EV** ,CHASSIS NO; **FE568EV532262** YEYOTE ATAKAEFANIKIWA KUIONA ATOE TARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAYE JALADA NAMBA **IRI/IRI/242436/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HELLEN DAUDI MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NISSAN SERENA** yenye usajili namba: **T 997 CUX,** CHASSIS NAMBA: **C25012939** na ENGINE NAMBA: **MR20056637A.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/242083/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**POPOTE ULIPO Ndugu, RAMADHAN JUMA MSEMO**
**KUITWA SHAURINI**
**Kesi ya madai No. 111 2023**

**Mdai: BENJAMIN JACOB ALEXANDER**
**Mdaiwa: RAMADHAN JUMA MSEMO**

Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Kariakoo kuja kusikiliza Shauri la Madai ya PESA No. 111/2023 siku ya ALHAMISI tarehe 11/8/2023 saa 2:30 asubuhi, kama utohudhuria shauri litasikilizwa upande mmoja.
Amri hii imetolewa leo tarehe 17 Mwezi wa 7 Mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Wamiliki na wakurugenzi wa kampuni ya **HODO QUALITY AND PERFOMANCE IMPROVEMENT ASSOCIATES LIMITED** yenye namba za usajili 136488, wanapenda kuutangazia umma kua kutokana na kushindwa kujiendesha,Wamiliki wameamua kuifunga kwa mujibu wa sheria za **BRELA.**

Hivyo tunaomba kama kuna mtu yeyote ana pingamizi, malalamiko au madai yoyote awasiliane kwa njia zifuatazo Email: **davisrumisha7@gmail.com**


**Davis Rumisha**
**Mkurugenzi Mtendaji23**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Athanas wilfred Masawe anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yake Aina ya Toyota cruger yenye namba za usajili **T 210 DQE**.
Taarifa imetolewa polisi simiyu **SM/MS/RB/241450/2023/.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi au awasiliane naye kwa namba **0754800500.**

**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED I, LATIFA RAMADHAN SAID of KITUNDA, DAR ES SALAAM. TANZANIA** formerly known as **LATIFA RAMADHAN CHIPALE.**
Do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former name of **LATIFA RAMADHAN CHIPALE** which was written in my **CITIZENSHIP INFORMATION** and in lieu thereof assume as from the name of **LATIFA RAMADHAN SAID** which was written in my **ACADEMIC CERTIFICATES**
**AND IN PURSUANCE** of such change of my name as aforesaid hereby declare that I shall at all-time hereinafter in all records, deeds and instrument: In writing and in all actions upon all occasions whatever use and sign the said name of **LATIFA RAMADHAN SAID** as my name in lieu of the former name of **LATIFA RAMADHAN CHIPALE** so renounced as aforesaid.
AND I hereby, authorize and request, all persons to designate and address me by such assumed name of **LATIFA RAMADHAN SAID** only.
I, the said **LATIFA RAMADHAN SAID** make this declarartion, conscientiously believing to be the same and in accordance with the provisions of the "Oaths".
IN WITNESS thereof I have executed this deed on the 10 of July 2023.



## KUPOTEA KWA VYETI



MEBO EZEKIEL KANYABUHA anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0202-0108 kilichotolewa na Bwiru Girls' Secondary mwaka 2008. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0586-0524 kilichotolewa na Kaisho Sekondary mwaka 2011. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: CHD/RB/1198/2023.

*OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com*

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Maandamano yazuka upya Kenya shule zafungwa

**NAIROBI,** KENYA

SERIKALI Kenya imeagiza shule za msingi na upili zilizopo jijini Nairobi na Mombasa zifungwe ikieleza kuwa imechukua hatua hiyo baada ya kupata taarifa ya kijasusi kwamba kuna baadhi ya watu waliopanga kushambulia shule katika kaunti hizo kupitia maandamano yaliyoitishwa na upinzani.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Mambo ya Ndani Prof. Kithure Kindiki huku Waziri wa Elimu Ezekieli Machogu akibainisha kuwa watatangaza tena kuanza kwa masomo kwenye shule hizo baada ya kutathimini hali ya usalama.

Jana nchini Kenya kumeshuhudiwa tena mandamano katika maeneo tofauti yaliyoitishwa na kiongozi wa upinzani Raila Odinga ili kupinga gharama ya juu ya maisha.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya kimataifa miongoni mwa madhara mengine yaliyosababishwa na maandamano hayo ni watu wawili kujeruhiwa na risasi pamoja na maduka kufungwa.

Pia ilielezwa kuwa makabiliano kati ya waandamanaji na maofisa wa polisi yalishuhudiwa katika eneo la Kibra mjini Nairobi, hali inayotajwa kuwalazimu maofisa hao kutumia vitoa machozi kuwatawanya.

**Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya kimataifa miongoni mwa madhara mengine yaliyosababishwa na maandamano hayo ni watu wawili kujeruhiwa na risasi pamoja na maduka kufungwa.**

Ilibainishwa kuwa mjini Mombasa maofisa wa polisi walimkamata mtu mmoja mapema jana baada ya waandamanaji kuwasha matairi barabarani na kufunga barabara inayoelekea katika Bandari ya Kenya.

Vile vile, ilibainishwa kwamba mjini Kisumu, waandamanaji waliwasha matairi wakati maandamano yakianza, huku ikielezwa kuwa kumekuwa na idadi kubwa ya maofisa wa polisi waliopelekewa katika maeneo tofauti ya nchi ili kuimarisha usalama.

**BBC, VOA**

# Ufilipino kuboresha bandari Afrika Kusini

**MANILA,** UFILIPINO

VITUO vya Bandari ya Transnet (TPT) imechagua huduma za Kituo cha Kontena cha Kimataifa (ICTSI) kama mzabuni anayependekezwa kwa ubia wa kuendeleza na kuboresha kituo kikuu cha gati ya pili ya mjini Durban Afrika Kusini.

Ilielezwa kuwa ICTSI yenye makao yake makuu Manila nchini Ufilipino itashirikiana na TPT kwa miaka 25 kuendeleza na kuboresha kituo kikuu cha kontena cha Transnet, kushughulikia asilimia 72 ya matokeo ya bandari ya Durban na 46 ya trafiki ya bandari za Afrika Kusini.

Transnet ilisema kukamilika kwa mchakato huo kunatokana na idhini kutoka serikalini ambayo ilitolewa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMA).

ICTSI ni mojawapo ya waendeshaji wakubwa wa kontena duniani na inasimamia vituo 34 katika nchi 20 zikiwamo bandari ya nchini Australia, Indonesia, China, Meksiko na Brazili.

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Transnet, Portia Derby, alisema ushiriki wa sekta binafsi katika gati ya pili ni kichocheo kikuu cha kuweka upya bandari ya Durban kama kituo cha kontena.

"Tunafuraha kuwa na mshiriki wa kimataifa wa ICTSI aliyesimama kwenye bodi kuendesha mchakato huu," alisema na kuongeza;

"Ushirikiano na ICTSI utasaidia kuweka upya kituo kwa utendaji kazi bora zaidi na kusaidia wasimamizi katika kutoa usaidizi wa kiutendaji na kibiashara ili kufikia njia za simu za kimataifa za usafirishaji," alisema Derby.

Pia alisema hiyo sio tu itaboresha vifaa vinavyohusiana na kuhudumia bandari za Afrika Kusini, lakini itakuwa na sehemu kubwa katika kuchochea mauzo ya nje na uagizaji.

Alieleza kuwa Transnet inapanga kukuza uwezo wa sasa wa gati ya pili kutoka TEU milioni mbili hadi TEU milioni 2.8, (TEU ni kipimo cha ujazo katika vitengo vya makontena yenye urefu wa futi ishirini).

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa hiyo inawiana na mipango ya Mamlaka ya Kitaifa ya Bandari ya Transnet (TNPA) ya kuongeza uwezo wa sasa wa kontena katika bandari nzima ya Durban kutoka TEU milioni 3.3 hadi uwezo unaotarajiwa wa TEU milioni 11.4.

# Ziara Waziri Mambo ya Nje Marekani nchini China yaleta mafanikio

**Na Fadhili Mpunji**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Janet Yellen, amemaliza ziara yake ya siku nne nchini China, ambayo wachambuzi wa mambo ya kidiplomasia na hata Yellen mwenyewe, wanaseme kuwa ni ziara iliyopata mafanikio makubwa.

Ziara hiyo ni hatua nyingine ya Marekani katika juhudi zake kurekebisha makosa yake ya kukata mawasiliano na China baada ya ziara iliyofanywa na aliyekuwa Spika wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi, na nyingine iliyotajwa kuwa ni kupita Marekani kwa kiongozi wa kisiwa cha Taiwan, Tsai Ying Wen.

Kwa mujibu wa CMG Swahili, ziara Yellen ni ya pili ya Ofisa Mwandamizi wa Serikali ya Marekani, iliyofanyika chini ya mwezi mmoja baada ya ziara ya mwezi Juni ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken.

Hatua ya Marekani kutuma maofisa wake waandamizi kwenye ziara nchini China, inatokana na nchi hiyo kutambua ukweli kwamba kutokuwa na mawasiliano na China ni kujihujumu yenyewe, na ni kuhatarisha maslahi yake binafsi na hata ya dunia.

Yellen alisema kuna haja ya China na Marekani kuwasiliana kwa karibu na kuepusha hatari zozote zinazoweza kutokea kutokana na kutowasiliana. Yellen alisema dunia ni kubwa, ambayo inaruhusu uwepo wa nchi mbili kubwa zenye nguvu.

Umoja wa Ulaya na baadhi ya nchi kadhaa za Ulaya, zimetambua kuwa China ni nchi yenye nguvu kubwa kiuchumi duniani na haiwezi kupuuzwa. Ndio maana viongozi wa Umoja wa Ulaya na wengine wa nchi kubwa za Ulaya kama Ujerumani na Ufaransa, wamekuwa wakisisitiza kuwa sera ya Umoja wa Ulaya au sera ya nchi zao kuhusu China haitaamuliwa Washington, bali itaamuliwa kutokana na hali halisi ya sasa ya nchi zao na maslahi yao, na mweleko wa sasa na wa siku zijazo wa dunia. Sera ambayo inaonekana kuwa ni ya busara.

Marekani imefikia hatua ya kuanza kufuata njia ya Umoja wa Ulaya na hata nchi nyingine duniani, kufanya uhusiano na China.

Pamoja na kuwa ziara za Blinken na Yallen zinaonesha mabadiliko makubwa ya sera ya Marekani, ni wazi kuwa bado kuna tofauti na changamoto zinazoendelea kuwapo kati ya China na Marekani, ikiwamo Marekani kuzuia baadhi ya teknolojia za hali ya juu kuingia China kama vile chip ndogo za kompyuta, lakini mawasiliano ya karibu kati ya China na Marekani ni muhimu kati ya pande hizi mbili, na pia ni muhimu kwa uchumi na usalama wa dunia.


**SUKAH SECURITY CO.LTD AUCTION MART**

(WATU WA KAZI)

**NOTICE OF SALE AND INVITATION OF SEALED BIDS FOR SALES OF PROPERTIES**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** under the power contained in the law and Mortgage Deed and other powers enabling us to do so, We **SUKAH SECURITY CO. LTD of P.O.Box 10751, Mwanza,** duly appointed by the **NCBA BANK TANZANIA LIMITED** (the bank) to sell the mortgages properties "as is" by sealed bids; **DO HEREBY INVITE BIDS FROM THE GENERAL PUBLIC** for the outright purchase of the properties described in the table below.

| No. | Property Description | Location | Property Registration Owner | Bids Submission Date | Bids Opening Date |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Plot No. 362 Block D CT No. 28625 | Kennedy Musoma | Vedastus Mathayo | On 19th August 2023 before 10:00 Hours at the address below | On 19th August 2023 at 10:30 Hours at the address below. |
| 2. | Plot No. 1 Block B CT. No. 16829 | Mkendo Street Musoma | Mathayo Sons Enterprises | On 19th August 2023 before 10:30 Hours at the address below | On 19th August 2023 at 11:00 Hours at the address below. |
| 3. | Plot No. 9 & 7 Low Density Block K CT. No. 1186 & CT. No. 1861 | Old custom Area Musoma | Mathayo Manyinyi | On 19th August 2023 before 11:00 Hours at the address below | On 19th August 2023 at 11:30 Hours at the address below. |
| 4. | Plot No. 210 Block K CT. No. 6673 | Kitaji Area Musoma | Steven Marwa | On 19th August 2023 before 11:30 Hours at the address below | On 19th August 2023 at 12:00 Hours at the address below. |
| 5. | Plot No. 204 Block J CT. No. 2047 | Kamunyonge Area Musoma | Steven Marwa | On 19th August 2023 before 12:00 Hours at the address below | On 19th August 2023 at 12:30 Hours at the address below. |
| 6. | Plot No. 90 Block A CT. No. 13788 | Mwigobero Area Musoma | East Africa Fossills Company | On 19th August 2023 before 12:30 Hours at the address below | On 19th August 2023 at 1:00 Hours at the address below. |

**TERMS AND CONDITIONS:**

1. Bid must be submitted in sealed envelope clearly marked **"BID FOR THE PURCHASE OF VEDASTUS MATHAYO, MATHAYO SONS ENTERPRISES, MATHAYO MANYINYI, STEVEN MARWA, STEVEN MARWA, EAST AFRICA FOSSILLS COMPANY PROPERTIES** including full address of the bidder.
2. The successful Bidder shall be required to deposit 75% of the bid price within 24 hours from the date of the award and balance 25% of the bid price within 7 days from the date of the award or within such other time as we may prescribe; failure of which the offer shall be revoked forthwith and the 75% down payment shall be forfeited and the next highest bidder who meets the conditions may be awarded, or cancel the sale process altogether.
3. Bids must be submitted and shall be opened on the date and address described in the table above. Bidders are invited to attend opening ceremony event if they so wish.
4. The property is being sold on "AS IS" basis, the Bank and us shall have no further liability after the sale.
5. The interested parties will be allowed to inspect the property by prior appointment.
6. All the information contained in this advertisement is free from liability.
7. The successful bidder or otherwise shall be notified within a maximum of two [2] days after bid opening; either to his physical address or his email address, which shall be sufficient communication.
8. The Bank and we shall not be bound to accept the highest bid or any bid at all or reject any or all the bids without having to assign any reasons.
9. All costs regarding transfer of ownership shall be borne by the successful bidder.
10. All bids shall be addressed to the address below.

**For further information please contact:**
**Managing Director, Sukah Security Company Ltd, Auction Mart**
**P.O.Box 10751 DVN Bldg.**
**Postal Road – Mwanza**
**Mob: 0754 860 435, 0715- 860 435**
**Email: sukahsecurity@gmail.com**

HABARI MICHEZO

# MAJALIWA AWATIA MORALI NAMUNGO FC

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya Namungo FC ya Ruangwa mkoani Lindi kufanya vibaya msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara, mkakati umeandaliwa kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri msimu huu na kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa ngazi ya klabu Afrika.

Msimu uliopita Namungo ilimaliza ligi katika nafasi ya tano ikiwa na pointi 40 na kukosa tiketi ya kuiwakilisha Tanzania katika michuano ya kimataifa ngazi ya klabu Afrika ambayo Tanzania itawakilishwa na Simba, Yanga katika Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Azam na Singida Fontain Gate zitacheza Kombe la Shirikisho.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini mkataba wa kuidhamini timu hiyo na Kampuni ya Insignia Ltd, watengenezaji wa rangi za Coral Paints pamoja na uzinduzi wa jezi mpya za msimu ujao, mlezi wa timu hiyo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema wanayataka mashindano hayo na wamejipanga vizuri kwa msimu ujao.

Huku akishangaliwa na mamia ya mashabiki wa Namungo kwenye Uwanja wa Majaliwa, Waziri Mkuu alisema kazi imeshaanza ambapo kwa sasa tayari wameipeleka timu kambini mkoani Manyara, huku wakiendelea na usajili wa kimyakimya na umakini kuhakikisha wanapata wachezaji wazuri wa kuisaidia timu hiyo.

Waziri Mkuu ambaye hata hivyo, alionyesha wasiwasi wa nafasi mbili za juu kuwa ngumu ikiwamo kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, amesema watapambana kuhakikisha wanaingia kwenye nne bora pamoja na kutwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho.

"Zile nafasi mbili za juu zinaweza kuwa mgogoro kwetu, japokuwa tutapambana na ipo siku tutafanikiwa kutwaa ubingwa na ndio malengo yetu," alisema.

"Lakini nafasi hii ya tatu na nne huku hatuna wasiwasi nayo, hii tunaiweza na tutapambana kwelikweli ili tucheze michuano ya kimataifa," alisema Waziri Mkuu.

Aidha, aliwashukuru wadhamini Coral Paints, akisema wameipa heshima Namungo kwa ujumla kupitia michezo.

"Tunawashukuru sana, mara ya kwanza mmetusaidia kukarabati uwanja na sasa mmekuja na udhamini ili kutupa nguvu katika safari yetu ya mafanikio,"alisema Majaliwa, ambaye ni Mbunge wa Ruangwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Insignia, Isaac Kiwango ambaye hata hivyo hakuweka wazi thamani ya udhamini huo, alisema udhamini wa kampuni hiyo ni wa miaka mitatu na umejikita katika maeneo mbalimbali na utakuwa wenye maboresho.

Alisema kampuni yake imedhamini vifaa vya timu hiyo ikiwemo jezi aina tano ambazo timu hiyo imezizindua ikiwa ni kwa ajili ya mechi za nyumbani, ugenini, kirafiki, Kombe la Shirikisho (FA) na nyingine ya kuitangaza Namungo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Namungo, Twaha Mpembenwe naye alisema wanataka kuona Namungo inafanya vizuri katika Ligi Kuu, Kombe la Shirikisho (FA) na hata itakaposhiriki michuano ya kimataifa.



Mchezaji wa Timu ya Chembe FC, Adam Mikidadi (kulia), akiwania mpira na wa timu ya Tumaini, Chacha Mwitta, katika mechi ya kirafiki iliyochezwa jana Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Mexime ataka mastaa Kagera Sugar

**Na Abdallah Mataka**

KOCHA wa Kagera Sugar, Mecky Mexime amesema kikosi chake kinahitaji wachezaji wakubwa 'mastaa' kwa ajili ya kukiboresha kikosi chake kuelekea kwenye msimu mpya wa ligi kuu.

Kauli hiyo ya Mexime imekuja siku mbili tu baada ya timu hiyo kuingia kambini kujiandaa na msimu mpya utakaoanza Agosti 15.

Kikosi cha Kagera Sugar kinafanya mazoezi yake kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Kaitaba mjini Bukoba.

Akizungumza kwenye mahojiano na kituo kimoja cha Redio, Mexime alisema anaendelea kusaka wachezaji ambao wataongeza nguvu katika kikosi hicho msimu huu na anataka wachezaji wenye uwezo utakaowasaidia.

"Kila timu naona inafanya usajili hata mimi nafanya pia katika maeneo ambayo nahitaji, usajili wangu hasa ni utalenga washambuliaji na mabeki kutokana na hali ilivyokuwa katika timu yetu msimu uliopita," alisema Mexime.

Alisema tayari kuna wachezaji wameanza kufanya nao mazungumzo na mambo yakikamilika watakuwa ndani ya kikosi hicho msimu ujao.

"Msimu uliopita timu yangu iliruhusu mabao 36 yakufungwa na tulifunga 23 hiyo inaonyesha kabisa kuna upungufu mahali na ndio maana tumekaa na wenzangu katika benchi la ufundi na kujadiliana, tutahakikisha msimu ujao tunaweka mambo sawa," alisema Mexime.

Kagera Sugar kuelekea msimu ujao tayari imeachana na wachezaji watano ambao ni Abeid Athumani, Yusuph Dunia, Meshack Mwamita na Erick Mwijage huku ikihusishwa kuwania saini ya mshambuliaji wa zamani wa Ihefu FC, Obrey Chirwa raia wa Zambia.

## Kipagwile atua Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji imeendelea na harakati zake za kukiboresha kikosi cha msimu ujao na sasa imenasa saini ya winga Idd Kipagwile kutoka Ihefu FC.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema imemsajili winga huyo kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu akiwa mchezaji wa tatu kusajiliwa mpaka sasa kati ya saba iliokusudia kuwaongeza msimu huu.

Kabla ya Kipagwile, ambaye ni mchezaji wa zamani wa klabu za Azam FC, KMC, na Namungo, Dodoma Jiji iliwatangaza wachezaji kutoka Coastal Union, Simon Gustapha ambaye ni beki wa pembeni na kiungo mkabaji, Mtenje Albano.

Mwenyekiti wa Kamati ya usajili wa Klabu hiyo, Fredrick Mwakisambwe, amesema usajili huo unafanywa kwa matakwa ya benchi la ufundi chini ya Kocha Melis Medo ambaye alitoa maelekezo baadhi ya maeneo yafanyiwe kazi.

"Tunaendelea na usajili hususani kwa wachezaji ambao wanatoka nje ya timu yetu kwa maana ya wageni, tumesajili wachezaji Mtenje na Gustavo kutoka Coastal Union na sasa tumempata Kipagwile, naamini atatuongezea nguvu kwenye kikosi chetu, kama nilivyosema hatutosajili wachezaji wengi, tumeamua kuongeza saba tu, lakini tumewaongezea mikataba wachezaji wetu waliopambana kuibakisha timu Ligi Kuu," alisema Mwakisambwe.

## Ligi Netiboli Z'bar yatimua vumbi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu ya Mpira wa Pete (Netball) Zanzibar imeanza kutimua vumbi jana kwenye viwanja vya Gymkhana mjini Unguja na kushirikisha timu tano.

Katika mchezo wa ufunguzi timu ya KVZ iliumana na Zimamoto na KVZ kufanikiwa kuibuka na ushindi wa magoli 51-35.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa Chama cha Mpira wa Pete Zanzibar (CHANEZA), Said Mansab, alisema uchache wa timu kwa msimu huu umetokana na mabadiliko ya kikanuni ya kundesha mashindano mbalimbali ya mchezo huo.

Alisema kuwa CHANEZA imezingatia vigezo vya kikanuni kama inavyotakiwa kwa timu ili iweze kushiriki mashindano mbalimbali ya ndani na nje huku baadhi ya timu zikishindwa kufikia vigezo hivyo.

Alisema miongoni mwa vigezo vinavyohitajika kikanuni ili iweze kushiriki Ligi hiyo ni kufanya usajili wa kudumu kwa wachezaji katika vilabu vyao na pia kuhakikisha timu inasajiwa kwa Ofisi ya Mrajisi wa vyama vya michezo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inafikiria kumnunua beki wa Manchester United na England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30. Beki wa The Blues Mfaransa Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 22, huenda akakaa nje ya uwanja kwa muda mrefu baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti. **(90 min)**

### BARNES AKARIBIA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inaweza kukamilisha dili la kumnunua winga wa Leicester City na England, Harvey Barnes siku chache zijazo na kuwasili kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kunaweza kumaanisha mshambuliaji wa Ufaransa, Allan Saint-Maximin kuondoka hapo Magpies. **(Mail)**

### MAXIMIN AWANIWA AL-AHLI

KLABU ya Al-Ahli inamtaka Saint-Maximin na wamepatia Newcastle United ofa ya euro milioni 25 kwa ajili ya mchezaji huyo. **(L'Equipe)**

### DIAZ AWINDWA ARABUNI

KLABU ya Saudi Arabia, Al-Hilal inavutiwa na mshambuliaji wa Liverpool, Luis Diaz lakini kuna uwezekano kuwa Wekundu hao watakubali euro 50 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia mwenye umri wa miaka 26. **(Record)**

### RAIS PSG AMCHUNIA MBAPPE

RAIS wa Paris St-Germain, Nasser Al-Khelaifi alimuona Kylian Mbappe kwenye uwanja wa mazoezi wa klabu hiyo Jumanne, lakini aliamua kutofanya mazungumzo ya ana kwa ana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. **(Sky Sports)**

### DIABY ATAKIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa imeweka dau lililoboreshwa la hadi pauni milioni 42.9 kumnunua winga wa Bayer Leverkusen na Ufaransa, Moussa Diaby. **(Athletic)**

### MAN OFA KWA HOJLUND

KLABU ya Manchester United itawasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Atalanta na Denmark, Rasmus Hojlund mwenye umri wa miaka 20, lakini klabu hiyo ya Italia itakataa euro milioni 70. **(ESPN)**

### MARSEILLE NA AUBAMEYANG

MARSEILLE inajiandaa kufanya mazungumzo na Chelsea kuhusu Pierre-Emerick Aubameyang, baada ya kufikia makubaliano ya kumsajili kwa mkataba wa miaka mitatu mshambuliaji huyo wa Gabon mwenye umri wa miaka 34. **(Guardian)**

### GALLAGHER MIL. 40

CHELSEA inataka zaidi ya pauni milioni 40 kwa Connor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, huku West Ham ikipania kumleta kiungo huyo wa kati wa England katika Uwanja wa London. **(Sky Sports)**

### KIMMICH KUUZWA

KLABU ya Bayern Munich iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich wakipokea ofa sahihi kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. **(Kicker)**

### TELLES KUHAMIA AL-NASSR

MLINZI wa Manchester United, Alex Telles anakaribia kuhamia klabu ya Saudi Arabia, Al-Nassr, huku klabu zote mbili zikizungumza kuhusu Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 30. **(Athaletic)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# JOAO FELIX ANATAKA KUJIUNGA BARCELONA

●●●Ningependa kuichezea Barca," alisema akimwambia mwandishi wa habari za michezo...

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Joao Felix amethibitisha nia yake ya kutaka kujiunga na Barcelona huku akijaribu kuondoka kwenye uwanja wa Wanda Metropolitano.

Felix alijiunga na Chelsea kwa mkopo kwa kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkataba wa bei ghali ambao haukuwa na chaguo la kumnunua na baada ya kufunga mabao manne katika mechi 20, The Blues hao walikataa kumsajili kwa mkataba wa kudumu.

Sasa amerudi Atletico, na 90min anaelewa kuwa Felix amesisitiza nia yake ya kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto na sasa ameitaja Barcelona kama kivutio chake cha ndoto zake.

"Ningependa kuichezea Barca," alisema akimwambia mwandishi wa habari za michezo, Fabrizio Romano.

"Barcelona daima imekuwa chaguo langu la kwanza na ningependa kujiunga na Barca.

"Siku zote ilikuwa ndoto yangu tangu nikiwa mtoto. Ikitokea, itakuwa ndoto yangu imetimia."

Ripoti kutoka Hispania zinasema kwamba Barcelona walifikia makubaliano ya kumsaini Felix mnamo Januari 2022, na kukubali kulipa ada ya euro milioni 70 ya awali na nyongeza ya euro milioni 65, ili tu kanuni za Financial Fair Play ziwazuie.

Felix alikaa kwa miezi 12 zaidi pale Atletico kabla ya kujiunga na Chelsea na sasa anataka klabu mpya.

Paris Saint-Germain inasemekana kuwa wanashughulikia mpango wa kumsajili Felix, ambaye thamani yake inakadiriwa kuwa euro milioni 90 - ada ambayo bila shaka itakuwa kubwa sana kwa Barcelona kumtwaa.

PSG wanaangalia mkataba wa mkopo na chaguo la kumnunua Felix moja kwa moja, lakini Atletico wanataka kumuuza na sio kwa mkopo.

# ARTETA: ARSENAL IMEJIPANGA UEFA



**WASHINGTON, Marekani**

KOCHA Mikel Arteta amesema kujengwa upya kwa Arsenal majira haya ya joto kutawasaidia kushindana tena kuwania taji la Ligi Kuu ya England, lakini hilo pia lilifanywa kwa kurejea kwa nguvu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Arsenal waliongoza jedwali la Ligi Kuu ya England kwa muda mrefu wa msimu uliopita, lakini kikosi cha Arteta hakikuweza kuizuia Manchester City ya kocha, Pep Guardiola katika wiki za mwisho za msimu na kumaliza nafasi ya pili.

Licha ya kutoshinda taji la nyumbani, Arsenal ilipata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2016-17 hali ambayo ililazimu mabadiliko makubwa kwenye kikosi.

"Itakuwa ngumu zaidi kwa hakika, kwa sababu ligi itaenda kwa kiwango tofauti tena, ambayo tayari ni ya kushangaza," alisema Arteta, ambaye alizungumza na ESPN huko Washington, D.C nchini Marekani, kabla ya mchezo wa timu yake dhidi ya MLS All- Stars jana Jumatano.

"Na ni wazi tuna hamu ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo hatujacheza kwa miaka mingi.

"Ndio maana tunahitaji kikosi tofauti na kile tulichokuwa nacho mwaka jana, nadhani tulichofanya msimu huu wa joto kinahusiana na hilo na ubora zaidi pia, bila shaka."

Wachezaji wawili wakubwa walioongezwa Arsenal msimu huu wa joto ni kiungo Declan Rice na mshambuliaji Kai Havertz.

Arteta alimmwagia sifa zake Rice, ambaye alisajiliwa kutoka West Ham kwa ada ya rekodi na Havertz, mchezaji wa zamani wa Chelsea na Bayer Leverkusen.

"Havertz ni mchezaji ambaye nimekuwa nikimpenda kwa muda mrefu na tulikuwa na uwezekano wa kumleta klabuni. Tulikuwa na mazungumzo machache kuhusu jinsi alivyokuwa anahisi kuhusu hilo na nilikuwa na hakika kwamba alikuwa aina ya mchezaji tuliyemtaka ili atupeleka mbele."

"Rice analeta uongozi, analeta sifa maalum ambazo hatukuwa nazo kwenye safu yetu ya kiungo. Ni wazi, ana uzoefu mzuri kwenye ligi, tayari amefanya mengi akiwa na umri wa miaka 24, lakini ana kitu."

Rice na Havertz wanajiunga na wachezaji wa kufurahisha pale Emirates akiwamo Bukayo Saka, Martin Odegaard na Gabriel Jesus, na Arteta aliongeza kuwa wachezaji wapya wa timu hiyo waliajiriwa sio tu kwa ajili ya vipaji vyao, bali pia kwa sababu walikuwa wanafaa kitamaduni kwa Arsenal.

# Pochettino: Lukaku hatumhitaji Chelsea

**NORTH CAROLINA, Marekani**

MAURICIO Pochettino amethibitisha kuwa anatarajia Romelu Lukaku kuondoka Chelsea msimu huu wa joto na amesema klabu hiyo inalenga kumsajili kiungo wa kati, lakini huenda isajili beki wa kati kutokana na majeraha mabaya ya Wesley Fofana.

Katika mahojiano yake ya kwanza ya kipekee tangu awe kocha wa Blues Julai Mosi, Pochettino aliiambia ESPN kazi ambayo Chelsea wamebakiza kufanya katika soko la usajili.

Lukaku hakuwa sehemu ya kikosi cha wachezaji 29 kilichosafiri hadi North Carolina siku ya Jumatatu kwa mechi tano za kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani wakianza na mechi ya kirafiki dhidi ya Wrexham jana Jumatano.

Juventus na Inter Milan wana nia ya kumsajili Lukaku na ingawa hadi sasa amekataa nia ya kutoka Mashariki ya Kati ya kujiunga na Ligi Kuu ya Saudi Aarabia, Saudi Pro League na Pochettino alisema kuwa mshambuliaji huyo anaona mustakabali wake kwingine baada ya mazungumzo na klabu hiyo.



Alipoulizwa na ESPN kama Lukaku anaondoka Chelsea, Pochettino alisema: "Nadhani ni dhahiri.

"Ni dhahiri kinachoendelea kwake. Nadhani kati ya klabu na mchezaji, wana mawazo sawa na tunafanyia kazi hilo ili kujaribu kurekebisha na kuwa na suluhu bora kwa pande zote mbili."

Pochettino alikiri kuwa jeraha la Fofana linaweza kuwalazimisha kuingia sokoni tena.

Klabu hiyo ilithibitisha katika taarifa yake kwamba Fofana alifanyiwa upasuaji wa kurekebisha goti na sasa anatarajiwa kuwa nje kwa muda mrefu.

"Angalia kilichotokea kwa Fofana," alisema Pochettino. "Labda ndio au hapana tunahitaji kufanya kazi kuchukua nafasi yake, wazo ambalo hatukuwa tunalifikiria. Hilo labda limetufanya kubadili mwelekeo.

"Lakini kama mpira wa miguu, ni kubadilika na mawazo ambayo unabadilisha. Kitu kinapotokea, unahitaji kuwa na umakini. Tunafanya kazi, kujaribu kuboresha. Hadi mwisho, tutakuwapo na tutaona kitakachotokea sokoni."

# Brighton yakataa ofa ya pili kwa Caicedo

**LONDON, England**

KLABU ya Brighton imekataa ofa ya pili kutoka kwa Chelsea kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati, Moises Caicedo.

Ofa ya hivi karibuni ya The Blues kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ecuador inaaminika kuwa inafikia karibu pauni milioni 70.

Caicedo aliomba kuondoka klabuni hapo Januari mwaka huu, huku Arsenal ikiwa na nia lakini Machi alisaini mkataba mpya hadi 2027.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye msimu uliopita aliwasaidia Seagulls hao kufuzu kucheza michuano ya Ulaya kwa mara ya kwanza na kufika nusu fainali ya Kombe la FA, bado anavutiwa na timu kadhaa za Ligi Kuu England.

Caicedo alijiunga na Brighton kutoka klabu ya Independiente del Valle ya Ecuador kwa kitita cha pauni milioni 4.5 Februari mwaka 2021 kabla ya kutolewa kwa mkopo kwa Beerschot ya Ubelgiji.

Alianza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Aprili 2022 na amecheza mara 53 wakati wake pale kwenye Uwanja wa Amex, akifunga mabao mawili.

Chelsea na Brighton zitamenyana Jumamosi hii mjini Philadelphia nchini Marekani katika mchuano wa kujiandaa na msimu mpya wa Ligi ya England unaojumuisha timu sita.



HABARI MICHEZO

# SINGIDA FG YAWEKA KAMBI ARUSHA

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Singida Fountain Gate kimewasili jijini Arusha kwa ajili ya kuweka kambi kujiandaa na msimu mpya wa mashindano wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya CAF.

Msimu ujao timu hiyo itaungana na Azam FC kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Wachezaji, benchi la ufundi na baadhi ya viongozi waliwasili jijini Arusha jana kwa maandalizi hayo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hussein Massanza alisema maandalizi hayo ya 'Pre Season' yatakuwa ya siku 14 kabla ya kurejea mjini Singida kwa ajili ya tamasha la kutambulisha wachezaji.

"Tunaweka kambi hapa kwa siku 14, programu ya mwalimu ni ya wiki mbili kwa mujibu wake tukiwa hapa, baada ya hapo tutarudi Singida kwa ajili ya tamasha la Singida Day, halafu tunaanza safari ya Tanga kwenda kwenye Ngao ya Jamii," alisema Massanza.

Mchezaji Deus Kaseke alisema wamefurahi kurejea tena jijini Arusha kwani hata msimu uliopita walifanyia 'pre season' kwenye jiji hilo.

"Kwanza hata msimu uliopita tulifanyia mazoezi hapa hapa, kwa hiyo tuna uzoefu napo, tutafanya maandalizi mazuri pamoja na hali ya hewa yake kuwa ya baridi sana naamini mambo yatakwenda sawa tu," alisema winga huyo wa zamani wa Yanga.

Aidha, Kiungo Yusuph Kagoma ametabiri msimu ujao kuwa mgumu, hivyo wanatakiwa kujiandaa kisawasawa ili kuweza kuipata tena moja kati ya nafasi za juu ya msimamo wa Ligi Kuu.

"Naona kama msimu ujao utakuwa mgumu sana kwa sababu timu nyingi zimejiandaa sana, zimesajili vizuri nadhani utakuwa msimu mzuri na mgumu sana, tunatakiwa kufanya maandalizi mazuri ili kupata tena moja kati ya nafasi nne za juu," alisema Massanza.

Singida Fountain Gate imecheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu uliomalizika na kufanikiwa kumaliza nafasi ya nne iliyoiwezesha kukata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akimkabidhi jezi ya Namungo mdhamini wa timu hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Insignia Limited, Isaac Kiwango, wakati wa kutangaza udhamini huo Ruangwa mkoani Lindi. **PICHA: OWM**

## Viongozi soka Zanzibar wateta na vilabu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

VIONGOZI wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mjini Magharibi (UWERFA) umefanya kikao na viongozi wa vilabu vitakavyoshiriki Ligi Daraja la Pili Mkoa wa Mjini Magharibi Msimu wa 2023/2014.

Lengo la kikao hicho ni kupitia kanuni za mashindano ya ligi hiyo na kufanya marekebisho ili kuweza kupata kanuni mpya ambayo itaongoza ligi hiyo Mkoa wa Mjini Magharibi kwa msimu wa 2023-24.

Ligi hiyo kwa msimu wa 2023/2024 inatarajiwa kuwa na timu 24 kutoka maeneo tofauti ya mkoa huo.

Timu zitakazomaliza katika nafasi mbili za juu zitapanda daraja na kucheza Ligi ya Kanda ya Unguja kwa msimu unaofuata 2024/2025.

Akizungumza na gazeti hili nje ya kikao hicho, Katibu UWERFA, Maalim Ahmada, alisema mabadiliko ya kanuni kwa kila msimu inatokana na changamoto ambazo zinajitokeza kwa msimu uliopita.

Alisema changamoto kubwa ipo kwa vilabu kwa kushindwa kusoma kanuni mapema badala yake kusoma kanuni pale wanapopata tatizo.

"Vilabu vyetu havioni umuhimu wa kusoma kanuni mpaka wapate adhabu, sasa hili nina tatizo timu inatakiwa isome kanuni yote kabla ya kuanza msimu ili kuhakikisha inajiepusha na adhabu wakati wa ligi," alisema Ahmada.

Alisema eneo kubwa lililofanyiwa marekebisho ni pamoja na kipengele cha adhabu ya timu itakayoshindwa kufika uwanjani kwa michezo mitatu.

"Kipengele hiki sasa kimefanyiwa marekebisho na timu ambayo haitakuwa imefika uwanjani mara tatu hata kama sio mfululizo itakutana na adhabu ya kushushwa daraja," alisema.

## Yanga yafunguka

INATOKA UK. 24

wao wapya.

Yanga itaadhimisha kilele cha Siku ya Mwananchi Jumamosi itakapocheza mchezo wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

"Nawaambia kuwa ngoma bado..., tunatarajia kushusha chuma kingine, tunataka tuhakikishe kwenye kilele cha Siku ya Wananchi Uwanja wa Benjamin Mkapa, watu wanakwenda kuangalia kiwango kikubwa kutoka kwa wachezaji wakubwa barani Afrika," Kamwe alitamba.

Ingawa klabu ya Yanga hawakusema wamemsajili kwa mkataba wa miaka mingapi, lakini habari za ndani zinasema mchezaji huyo mwenye miaka 33 amepewa mkataba wa mwaka mmoja.

Mchezaji hiyo aliyeanzia soka lake kwenye kikosi cha pili cha Mamelodi Sondowns, amezichezea klabu nyingi za Afrika Kusini zikiwamo United FC, Platinum Stars, Golden Arrows, Orando Pirates, Highlands Park, University of Pretoria na Marumo Gallants, kabla ya kujiunga na Yanga kwa ajili msimu ujao.

## Miquissone uhakika

INATOKA UK. 24

maneno haya kwenye mtandao wake wa instagram.

"Kijana amemalizana na klabu namba moja Afrika, haya sasa tuone anafanya nini?" Posti hii imewafanya mashabiki wengi kuamini kuwa Miquissone anarejea kwenye klabu ya Simba.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema mchezaji huyo alishamalizana na Simba muda mrefu kuhusu mshahara na mambo mengine, na kilichobaki ilikuwa ni Miquissone mwenyewe kwenda kuzungumza na Al Ahly kama atakwenda kwa mkopo, au vinginevyo na baada ya mazungumzo ya siku kadhaa, klabu hiyo na mchezaji wakaamua kuachana kwa amani.

Winga huyo raia wa Msumbiji ambaye Simba ilimsajili 2020 kutokea UD Songo ya Msumbiji alipokuwa akiichezea kwa mkopo kutoka Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, aliuzwa kwa kiasi kichopungua Sh. bilioni 2 kwenda Al Alhy 2021, lakini hakuwa na wakati mzuri kiasi cha kupelekwa kwa mkopo katika klabu ya Abha ya Saudi Arabia.

Wakati huo huo, wakati safari ya kuelekea kilele cha Mlima Kilimanjaro kutambulisha rasmi jezi za msimu ujao ikianza jana, uongozi wa Simba umeweka wazi kuwa bado watasajili wachezaji wengine watano wakiwamo wa kimataifa wawili na nafasi nyingine za wachezaji wazawa.

Katika nafasi hizo tano mpaka sasa mzawa Iddi Chilunda anatajwa kuwa mmoja wapo wanaotaka kusajiliwa huku wa kigeni, Miquissone na golikipa mmoja kutoka nje ya nchi wakitajwa.

Jana viongozi wa Simba waliusindikiza msafara wa wanachama walioteuliwa kwenda kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro kutambulisha jezi zao.

Msafara huo unatarajiwa kufika kileleni kesho na kutambulisha rasmi jezi hizo zitakazotumika msimu ujao kwenye mashindano ya kitaifa na kimataifa.

Michezo

Alhamisi Julai 20, 2023
Nipashe



## Joao Felix anataka kujiunga Barcelona

UKURASA 21

# Miquissone uhakika Simba, safari uzinduzi jezi yaanza

Adam Fungamwango (Dar) na Saada Akida, MOSHI

BAADA ya taarifa zilizotoka juzi jioni kuwa winga wake wa zamani, Luis Miquissone amevunja mkataba na klabu ya Al Ahly ya Misri, inaelezwa uongozi wa Simba upo katika hatua za mwisho za kumsajili nyota huyo.

Kwa muda mrefu uongozi wa Simba ulikuwa ukimwinda nyota huyo raia wa Msumbiji lakini ulikuwa haujafikia muafaka juu ya masilahi yake.

Taarifa za mchezaji huyo kuvunja mkataba na Al Ahly zilitoka juzi na Miquissone mwenyewe aliiposti barua hiyo ya makubaliano ya kuvunja mkataba kwenye mtandao wake wa kijamii wa 'instagram' ikieleza kumalizana na Al Ahly kwa kuvunja mkataba kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya mchezaji wao huyo wa zamani kufanya hivyo, ndani ya siku chache kila kitu kitafahamika.

"Tumesikia taarifa ya Miquissone kuvunja mkataba na kwetu sisi tunaichukulia kwa pande mbili, kwanza tumeumia kwa sababu kama Simba tunapomuuza mchezaji klabu kubwa tunataka akafanye vizuri, kwa sababu ni heshima kwetu, watu wakiuliza katoka wapi huyu na sisi tunatajwa, tulitaka afanye vyema ili tuzidi kuheshimika, angefanya vyema wangerudi tena kuchukua mchezaji mwingine, kwa upande huo imetuuma," alisema Ahmed.

"Kwa mtazamo wa pili tumefurahi kwa sababu kijana sasa yupo huru, maana yake anafungua milango ya watu ambao wanamhitaji kwenda kuzungumza naye, sasa kwa hili tuwaachie viongozi wakubwa wa Simba, wataamua kama wanamchukua ama la, lakini kila mmoja anatambua ubora wa Miquissone na ndani ya siku chache kila kitu kitafahamika," alisema Ahmed.

Naye Mwekezaji na Rais wa Heshima wa Klabu hiyo, Mohamed Dewji, baada ya barua hiyo kutoka aliandika

INAENDELEA UK. 23



Nyota mpya wa Yanga, Mahlatse Makudubela 'Skudu' (kulia), wakati akiwa na klabu yake ya Marumo Gallants akipambana na beki wa Yanga, Kibwana Shomari, walipokutana kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAFUNGUKA UJIO MAKUDUBELA 'SKUDU'

●●●Yasema sasa jezi namba sita imepata mrithi sahihi, atabiriwa kutawala eneo la...

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema sasa jezi namba sita iliyoachwa na Feisal Salum 'Feitoto' imempata mrithi na ni 'mrithi sahihi' kutoka klabu ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini.

Jana Yanga ilitangaza kukamilisha usajili wa kiungo Mahlatse Makudubela 'Skudu' ambaye anakuja kuchukua nafasi ya Feitoto aliyetimkia Azam FC.

Kwa muda mrefu tangu kufunguliwa kwa dirisha la usajili, Yanga walikuwa wakinadi jezi namba sita kuwa inakuja kurithiwa na mchezaji mkubwa.

Juzi usiku, klabu hiyo ilimtangaza mchezaji huyo raia wa Afrika Kusini kuwa sasa ni mchezaji wao rasmi, akipewa jezi namba sita.

Akizungumza jana, ofisa habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema wamemsajili mchezaji mwenye kiwango cha hali ya juu na fundi wa mpira, hivyo kwa sasa mashabiki wa Yanga watakapokuwa wamekwenda uwanjani, siyo tu watafurahia kushinda, lakini watapata raha kuona namna anavyolisakata kabumbu.

"Kiu ya wananchi ya jezi namba sita imemalizwa ipasavyo, unaona jinsi wanachama na mashabiki walivyompokea Makudubela ' Skudu Master', kijana mwenye kipaji na kuonyesha kuwa msimu ujao si tu kwamba tunashinda, bali tunashinda kwa kupata raha," alisema Kamwe.

Kamwe alisema wanamatumaini makubwa na mchezaji huyo kutokana na rekodi na ubora wake na wanaamini atakuja kutawala eneo la katikati la timu hiyo.

Alisema aina ya usajili wanaoufanya kwa sasa ni wa kiwango cha juu na lengo ni kuendeleza ufalme wa soka nchini lakini kufika hatua za juu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika msimu ujao.

"Hatuna masihara hata kidogo msimu ujao tunataka tufike kwenye ngazi za juu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, pia tunataka tuendeleze ufalme wetu ligi ya ndani ndiyo maana tunafanya usajili bora," alisisitiza.

Ofisa Habari huyo aliendelea kusema kuwa usajili bado unaendelea na wanatarajia kumtangaza mchezaji mwingine wa kigeni, huku akiwataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kumiminika kwa wingi, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jumamosi ijayo kuwaangalia wachezaji

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042